epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710 LIKE & FOLLOW US
Jumamosi Desemba 7, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581883
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**MUSIALA KUSAINI MKATABA MPYA BAYERN MUNICH**

UKURASA WA 2

**Tozo** 370 zafutwa kuimarisha mazingira biashara, uwekezaji

UKURASA WA 2

**Afariki** kwa kuangukia sime akisherehekea kufanyiwa tohara



UKURASA WA 3

**Mdude** apata dhamana baada kusota rumande kwa siku 10

# Simulizi wananchi kipigo kwa maofisa TRA madai watekaji

• **Mwenye** gari aliyedaiwa kutekwa matatani, Waziri Nchemba alaani... *Uk.2*



"Tunamshikilia dereva aliyepiga kelele akidai anatekwa kwenye tukio lililosababisha wananchi kuwajeruhi watumishi wa TRA pamoja na gari.

**SACP Muliro**



"Wakati watumishi hao wanatimiza wajibu wao, walihusishwa na kitendo cha utekaji, kilichosababisha wao na gari kushambuliwa.

**Richard kayombo**



"Nimesikitishwa na tukio la kushambuliwa kwa watumishi wa TRA na gari lao walipokuwa wakitekeleza majukumu yao.

**Dk. Nchemba**

"Huyu dereva aliyekuwa anafuatiliwa na hawa watu, alipowadai kitambulisho ili kujua kama ni kweli watumishi wa TRA, sikuona kama wametoa, ndipo yule dereva wa gari dogo akaanza kupiga kelele na kusema, 'hawa si watu wa TRA, ni watu wasiojulikana, sijui wanataka kunipeleka wapi.

**Shuhuda**

## Kizimbani madai ya kumteka Tarimo

UKURASA 3



## Chanzo ajali wabunge, kujeruhiwa chaanikwa

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA: TUTABEBA POINTI TATU MUHIMU** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Simulizi wananchi kupiga maofisa TRA wakidaiwa watekaji

**Romana Mallya na Tuntule Swebe**

WAKATI kukiwa na sintofahamu ya matukio ya utekaji yanayodaiwa kufanywa na watu wasiojulikana, katika hali isiyotarajiwa watumishi watatu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wamejeruhiwa wakihusishwa na utekaji, katika jaribio lao la kumkamata dereva barabarani.

Tukio hilo lilitokea juzi jioni eneo la Tegeta kwa Ndevu, wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, baada ya dereva aliyekuwa akifuatiliwa na TRA kusababisha watumishi wake wapigwe mawe kwa madai ni watu wasiojulikana.

**ILIVYOKUWA**

Baadhi ya mashuhuda ambao hawakutaka majina yao kuandikwa gazetini, walisimulia tukio hilo lilivyotokea, wakidai lilitokea wakati watu hao (watumishi TRA) wakikimbiza gari la raia.

Walidai wakati wakilikimbiza gari hilo lililokuwa mbele yao baada ya kufika Tegeta, walilizuia na ndipo dereva huyo aliposhuka.

Mmoja wa madereva wa pikipiki ambaye alishuhudia tukio hilo (jina linahifadhiwa), alidai kuwa baada ya mtu huyo kuwahoji kwa nini wanamfuatilia, watu hao walijitambulisha kama watumishi wa TRA.

"Huyu dereva aliyekuwa anafuatiliwa na hawa watu, alipowadai kitambulisho ili kujua kama ni kweli watumishi wa TRA, sikuona kama wametoa, ndipo yule dereva wa gari dogo akaanza kupiga kelele na kusema, 'hawa si watu wa TRA, ni watu wasiojulikana, sijui wanataka kunipeleka wapi'.

Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa Tegeta, Bered Ntabaliba, alisema, akiwa nyumbani kwake majira ya saa 4:00 usiku, alipokea simu ya kuitwa aende barabara ya Kwa Masista kwamba kuna watu wasiojulikana wanapigwa.

Alisema alipofika eneo la tukio, alikuta kuna majeruhi mawili na mmoja ameshaondoka maeneo hayo kulikokuwa na watu wengi, ndipo alipowasiliana na polisi.

"Wakati tuko na polisi eneo la tukio, mwananchi alirusha jiwe na kumpata askari polisi mmoja eneo la jicho. Tulipoona vurugu zinazidi, tuliingia katika bajaji na kuwachukua majeruhi na kuwapeleka Hospitali ya Kitengule.

**MOI YAPOKEA MAJERUHI**

Ofisa Uhusiano wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Abdallah Nassoro, aliliambia Nipashe jana walipokea majeruhi wawili wa tukio hilo.

Aliwataja kuwa ni Adranico Alfred (30) ambaye alitibiwa na kuruhusiwa na mwenzake, Amani Kamguna (37) ambaye amepata majeraha makubwa kichwani na kufanyiwa operesheni.

**TRA YAFAFANUA**

TRA kupitia Idara ya Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano ilitoa ufafanuzi kuhusiana na tukio hilo lililohusisha watumishi wake.

"TRA inasikitika kuutarifu umma kwamba, gari yake lenye namba za usajili STL 9923, Ikiwa na watumishi watatu katika doria za kawaida za udhibiti na ukamataji wa magendo na magari yaliyoingia nchini kinyume cha taratibu za forodha na kutolipiwa ushuru, limeshambuliwa na watumishi kuumizwa katika eneo la Tegeta kwa Ndevu jana usiku.

Kadhia hii imetokea baada ya watumishi wa TRA kubaini kwamba, gari namba T 229 DHZ aina ya BMW X6 iliyoingizwa nchini kinyume bila kulipa kodi za serikali stahiki kwa mujibu wa sheria na kuifuatilia kwa lengo la kuikamata, ili kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria za kodi.

"Wakati watumishi hao wanatimiza wajibu wao, walihusishwa na kitendo cha utekaji, kilichosababisha wao na gari kushambuliwa.

**DK. MWIGULU ALAANI**

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, kupitia ukurasa wake wa Instagram jana, aliandika maneno yanayosomeka: "Nimesikitishwa na tukio la kushambuliwa kwa watumishi wa TRA na gari lao STL 9923 walipokuwa wakitekeleza majukumu yao ya kisheria ya kudhibiti magendo na magari yaliyoingizwa nchini kinyume cha sheria."

**KAULI YA POLISI**

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, alinukuliwa na baadhi ya vyombo vya habari kwamba, wanamshikilia dereva aliyepiga kelele akidai anatekwa kwenye tukio lililosababisha wananchi kuwajeruhi watumishi wa TRA pamoja na gari.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Afa kwa kuangukia sime akisherehekea tohara

**Na Ambrose Wantaigwa,** SERENGETI

WATU wawili wamefariki dunia, mmoja baada ya kuangukia sime yenye makali wakati akisherehekea tohara na mwingine ameuwawa na mwanawe alipomkataza asiuze maharage ya mbegu.

Katika tukio la kwanza, Jeshi la mkoani Mara linamshikilia, Gesoreka Mabula (30), mkazi wa Kijiji cha Mesega, wilayani Serengeti, kwa tuhuma za kumuua baba yake mzazi kwa kumchinja kisa ugomvi wa kifamilia.

Kamanda wa Polisi mkoani humo, SACP Pius Lutumo, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana mjini Musoma na kwa kushirikiana na wasamaria wema walimkamata mtuhumiwa huyo katika eneo la Majimoto akiwa katika harakati za kutoroka.

SACP Lutumo alimtaja marehemu kuwa ni Mabula Mwita (61) ambaye alifariki dunia kutokana na kuvuja damu nyingi zilizotokana na kukatwa na kitu chenye ncha kali shingoni.

"Inadaiwa kuwa juzi (Desemba 5) saa 12.00 alfajiri katika Kijiji cha Mesega, Kata ya Kenyamonta, wilayani Serengeti, mtuhumiwa alimuua baba yake kwa kumkata na kitu chenye ncha kali shingoni upande wa kushoto na baada ya kutenda tukio hilo alikimbia," alisema SACP Lutumo.

Alisema baada ya kupokea taarifa hizo, Jeshi la Polisi lilianza msako kwa kutumia taarifa fiche kutoka kwa wasamaria wema na kuweka mitego na kumkamata mtuhumiwa huyo akiwa mafichoni.

Alisema chanzo cha mauaji hayo ni baada ya baba yake kumzuia mtuhumiwa kuchukua maharage yaliyohifadhiwa kwa ajili ya mbegu, ili kwenda kuyauza.

Mmoja wa majirani wa familia hiyo, Abel Marwa, alisema kwa muda mrefu mtuhumiwa huyo alikuwa akijihusisha na ugomvi wa mara kwa mara na mzazi wake huyo ambaye sasa ni marehemu.

Katika tukio la pili, mkazi wa Kitongoji cha Nyaihunyo, Kijiji cha Gwitiryo, Tarafa ya Inchugu, Wilayani Tarime, mkoani Mara, Gesabo Dalimas, amefariki dunia kwa kukatika shingo baada ya kuangukia panga aina ya sime lenye makali pande zote alilokuwa ameshikilia wakati akisherehekea sherehe za tohara.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.t*



Abiria wa mabasi yaendayo haraka (BRT), wakiwa kwenye foleni kubwa ya kusubiri usafiri huo, katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam jana asubuhi. Kwa mujibu wa abiria hao, foleni hiyo inatokana na mabasi hayo kukwama kuingia kituoni hapo, kwa sababu ya msongamano wa daladala. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Tozo 370 zafutwa kuimarisha biashara, uwekezaji

**Na Restuta James**

SERIKALI imefuta tozo 374 na kurekebisha sheria na kanuni 55, huku zingine 16 zikiendelea kufanyiwa maboresho, ikiwa ni mkakati wa kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo jana Dar es Salaam alipokuwa akifungua Kongamano la Majadiliano ya Biashara na Uwekezaji Kati ya Serikali na Sekta Binafsi na Mkutano Mkuu wa 49 wa Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA).

Alisema kufutwa kwa tozo hizo kumepunguza Sh. bilioni 35 kwenye mapato ya serikali kwa mwaka na kwamba imefanya hivyo baada ya kusikiliza kero za wafanyabiashara.

Pia alisema serikali imepunguza muda wa kutoa huduma kutoka simu 14 hadi tatu na usajili wa hospitali binafsi, kutoka miezi 12 hadi siku tatu.

Alisema lengo la serikali kufanya hivyo ni kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

Dk. Biteko alisema serikali imefanya hivyo ili kuongeza mzunguko wa biashara ambao utaongeza mapato ya kodi, itakayotumika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na huduma za kijamii.

Alisema mbali na maboresho hayo, serikali imeimarisha bandari na miundombinu mingine, ikiwamo ujenzi wa barabara, meli, reli ya kisasa na ununuzi wa ndege ya mizigo.

Maboresho hayo, alisema yameongeza mahitaji ya umeme kutoka megawati 70.8 mwaka 2017/18, hadi megawati 420 mwaka huu.

"Mahitaji ya juu ya umeme Agosti mwaka jana yalikuwa megawati 1,410 lakini leo ni MW 1,888, ongezeko hili limekuja kwa sababu viwanda vingi vinajengwa na uchumi unachangamka," alisema.

Dk. Biteko alisema serikali inatambua mchango wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi na kuwashauri wanachama wa TCCIA, kutumia malighafi za ndani katika kuzalisha bidhaa zenye ubora, zitakazoweza kushindana sokoni.

"Mchango wa sekta binafsi ni mkubwa na hauwezi kupuuzwa. Vijana zaidi ya milioni 12 wanaingia kwenye soko la ajira kila mwaka, asilimia 25 ndio wanapata ajira katika sekta rasmi. Asilimia 75 wanaingia katika sekta isiyo rasmi mkiwamo ninyi," alisema Dk. Biteko.

Rais wa TCCIA, Vicent Minja, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuifungua nchi na kutatua changamoto za biashara.

Hata hivyo, aliomba mchakato wa kuandika sera ya sekta binafsi uharakishwe ili kuiweka kwenye mpangilio unaohitajika.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

# Chanzo ajali wabunge, watumishi chaanikwa

**Augusta Njoji na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani hapa limetaja chanzo cha ajali ya basi lililojeruhi wabunge, watumishi wa Bunge na watu wengine jumla yao 23 kuwa ni uzembe wa dereva kushindwa kuchukua tahadhari alipotaka kulipita gari lingine barabarani.

Kutokana na uzembe huo, Jeshi la Polisi linamshikilia kwa mahojiano dereva huyo, Bahati Saidi, kutoka Kampuni ya Shabiby, ambaye pia ni miongoni mwa majeruhi wanaoendelea na matibabu.

Jumatano ya wiki hii, Rais Samia baada ya kutokea ajali iliyohusisha magari matatu na kuua watu saba na kujeruhi tisa, alilielekeza Jeshi la Polisi kuhakikisha madereva wanaongeza umakini na kuzingatia sheria za barabarani, hasa kipindi hiki cha mwisho wa mwaka ili kuepusha ajali zinazoweza kuepukika.

Pia aliagiza uhuishaji na uwekaji wa alama za barabarani kwenye maeneo hatarishi na kuzingatia umbali na maeneo sahihi ya uwekaji wa vituo vya ukaguzi ili vionekane kwa urahisi zaidi.

Akizungumzia jana ajali hiyo ya wabunge, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi, alisema ilitokea saa 2:00 asubuhi katika barabara kuu ya Dodoma- Morogoro, eneo la Mbande, wilayani Kongwa.

Kamanda Katabazi alisema kati ya waliojeruhiwa, wabunge ni 17, maofisa wa Bunge wawili, askari wawili, dereva na kondakta.

Kamanda Katabazi alisema wabunge hao walikuwa wakisafiri kwenda Mombasa, Kenya kushiriki Mashindano ya 14 ya Mabunge ya Afrika Mashariki.

Alisema basi hilo limegongana uso kwa uso lakini dereva wa lori alijaribu kuchukua tahadhari ili wasigongane na alipanua kidogo njia ili kulipisha gari lililokuwa likipita lakini basi likagonga tela la lori.

Kwa mujibu wa SACP Katabazi, majeruhi hao walelazwa katika Hospitali ya Kanda za Rufani ya Benjamin Mkapa, Kongwa, Chamwino na wengine wamepelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa Dodoma na wanaendelea na matibabu vizuri na hakuna kifo chochote kilichotokea.

"Eneo hilo alilotaka kulipita gari hilo haliruhusiwi kupita gari lililo mbele.Kuna mistari ya katazo ya kutolipita gari lililo mbele yake lakini dereva hakuzingatia hilo na matokeo yake amesababisha ajali hiyo.

"Kama mnavyoona alitoka nje zaidi ya barabara baada kugonga tela hilo na kushindwa kulimudu gari na kutoka nje ya barabara zaidi ya mita 10 hadi 15," alisema.

Kamanda Katabazi alisema wanamshikilia dereva huyo kwa mahojiano zaidi na hatua nyingine za kisheria zitazingatiwa.

"Ajali hii imesababisha majeruhi na uharibifu wa magari. Kwa hiyo marereva wakizingatia sheria za usalama barabarani ajali zitaepukika. Ni muhimu wazingatie sheria kwa kuwa kilichotokea ni uzembe na kutozingatia sheria husika,"alisema.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano katika Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), Jeremiah Mwakyoma, alithibitisha kupokewa kwa baadhi ya majeruhi wa ajali hiyo na kwamba wanaendelea na matibabu huku hali zao zikiendelea vizuri.

Akizungumza mara baada ya kuwajulia hali majeruhi hao, Waziri wa afya, Jenister Mhagama, alisema wamepokea majeruhi 23 na wote wanaendelea vizuri.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Meneja wa Huduma za Jamii wa Benki ya NBC, Irene Peter (wa tatu kushoto), akikabidhi shehena ya taulo za kike boksi 153 kwa Ofisa Uhusiano wa IPP, Nancy Mwanyika, zilizotolewa na benki hiyo, kwa ajili ya kuunga mkono kampeni ya Namthamini inayoendeshwa na EATV/Redio, katika hafla Mikocheni,Dar es Salaam juzi, zitakazokwenda kusaidia zaidi ya wasichana 300 waliopo mashuleni. Wengine ni Meneja wa Uhusiano kwa Wateja wa benki hiyo, Theresia Assey (kushoto), Balozi wa Namthamini, Samson Charles (wa pili kushoto),Ofisa wa Benki hiyo, Nicole Kyakula (wa pili kulia) na Mtangazaji wa East Africa Radio, Rita Chuwalo. **PICHA: EATV**

# Kortini madai kumteka mfanyabiashara Tarimo

**Na Grace Gurisha**

VIJANA sita wakazi wa Dar es Salaam, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, wakikabiliwa na shtaka la kujaribu kumteka mfanyabiashara Deogratius Tarimo kwa lengo la kumweka kizuizini. Washtakiwa hao ni Fredrick Nsato (21), Isaack Mwaifwani (29), Benk Mwakalebela (40), Bato Tweve (32), Nelson Msela (24) na Anitha Temba(27).

Akisoma hati ya mashtaka, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu wa Mahakama hiyo, Ramadhan Rugemalila, Wakili wa Serikali, Jonh Mwakifuna, alidai kuwa watu hao wanakabiliwa na shtaka moja. Alidai kuwa washtakiwa hao wote walitenda shtaka hilo, Novemba 11, 2024 eneo la Kiluvya Madukani Lingwenye, Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam, walijaribu kumteka nyara Deogratius Tarimo kwa lengo la kumweka kizuizini. Baada ya kusomewa shtaka hilo, wote kwa pamoja walikana mashtaka hayo. Upande wa mashtaka ulidai upelelezi umekamilika na kuiomba mahakama kupanga tarehe ya usikilizwaji wa awali. Hakimu Rugemarila aliwaeleza washtakiwa hao kuwa shtaka lao lina dhamana, hivyo ili wawe nje kwa dhamana, kila mshtakiwa anatakiwa awe na wadhamini wawili watakaotia saini fungu la dhamana la Sh. Milioni 10 kwa kila mmoja.

Hakimu aliwataka kila mdhamini awe na barua ya utambulisho kutoka kwa mwajiriwa kwa aliyeajiriwa au barua kutoka kwa mtendaji kata ikiwa na mhuri wa Mkurugenzi wa Manispaa husika.

Pia aliwataka washtakiwa hao kutosafiri nje ya mkoa wa Dar es Salaam bila kibali cha mahakama. Washtakiwa wote walirudishwa rumande baada ya kushindwa kutimiza masharti ya dhamana na shauri liliahirishwa hadi Desemba 19, mwaka huu.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

## Mdude apata dhamana baada ya kusota mahabusu siku 10

**Na Moses Ng'wat,** MBOZI

MWANAHARAKATI mwenye ushawishi na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Mdude Nyagali, aliyekuwa akishikiliwa na Jeshi la Polisi kwa zaidi ya siku 10, amefikishwa mahakamani jana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kukamilika kwa taratibu za dhamana, Wakili Sambwe Shitambala, alilaani kitendo cha polisi cha kumshikilia Mdude kwa muda wote kuanzia Novemba 22 hadi jana, bila kumpatia dhamana dhidi ya tuhuma zinazomkabili.

"Ndugu yetu Mdude bahati nzuri amesomewa mashtaka yake leo (jana) na amedhaminiwa kwa sasa. Haki ya dhamana ni ya kila mwananchi ambayo kimsingi inatakiwa itolewe mapema iwezekanavyo.

"Lakini imechelewa na hili kama mawakili, kama Watanzania, tunalaani. Hatupendi kuona mwananchi ambaye analindwa na Katiba hana haki na uhuru anaostahili wakati sheria inampa haki ya kuwa huru kwa mujibu wa sheria ndogo zitakazotungwa kutokana na Katiba.

"Tumeona Mdude analetwa leo (jana) tangu siku anakamatwa, yaani wiki mbili zaidi baadaye kitendo ambacho si cha kistaarabu katika nchi ambayo ni huru, imesaini mikataba mingi ya kimataifa kuhusu raia na usimamizi wa haki za binadamu, si kitendo chema tusingependa kirudiwe", alisema.

Novemba 22, mwaka huu, Mdude alikamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Songwe katika Wilaya ya Mbozi na wenzake 11, akiwamo Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, wakidaiwa kufanya mkutano wa kampeni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika eneo ambalo hawakupangiwa na msimamizi wa uchaguzi.

Licha ya jeshi hilo kuwaachia wenzake 10, liliendelea kumshikilia Mdude huku akihamishiwa katika mahabusu mbalimbali za Mkoa wa Songwe na nje ya mkoa huo, akituhumiwa kwa makosa ya kusambaza taarifa za uongo mitandaoni, kutoa lugha za matusi na kujeruhi.

Hivi karibuni, mawakili wa Mdude wakiongozwa na Boniface Mwabukusi na Philip Mwakilima, walikuwa na maombi Mahakama Kuu ya Tanzania, Kanda ya Mbeya, wakitaka Mdude adhaminiwe au afikishwe mahakamani.

Mawakili hao waliokuwa waleta maombi, wameondoa shauri hilo mahakamani mbele ya Jaji Victoria Nongwa na mawakili wa Serikali Dominic Mushi na Lodgard Eliaman.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Makinda ataka utafiti wavulana kuachwa kitaaluma na wasichana

**Na Joseph Mwendapole**

SPIKA Mstaafu, Anne Makinda, amependekeza kufanyika utafiti kujua sababu za watoto wengi wa kiume kuachwa nyuma kitaaluma na wenzao wa kike.

Makinda ambaye pia ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Kairuki, aliyasema hayo jana wakati wa kongamano la sita kitaaluma lililoandaliwa na chuo hicho kujadili sekta ya afya inavyoweza kufanya mabadiliko kwa huduma hizo kutolewa kidijitali.

Alisema kwa siku za karibuni, watoto wa kike wameonekana kuongoza kitaaluma na kuwaacha mbali wenzao wa kiume jambo ambalo alisema jamii haipaswi kulifumbia macho na kuliona kama la kawaida.

"Hili si jambo la kawaida kabisa na tusilichukulie kirahisi. Lazima tutafute sababu za kwa nini hawa watoto wanaanguka kitaaluma. Lazima kuna sababu, kwa hiyo tukifanya utafiti, tutapata sababu na tutachukua hatua.

"Ni jambo jema kuona watoto wa kike wanakuwa mbele kielimu baada ya miaka mingi ya kuwa nyuma lakini si lengo letu kufurahia watoto wa kiume kuachwa nyuma. Tuwapongeze watoto wa kike lakini tujue tatizo ni nini. Tunaposema 50 kwa 50 tuna maana twende kwa usawa" alisema.

Makinda alisema hali hiyo haiko Tanzania pekee bali katika mataifa mbaalimbali watoto wa kiume wameanza kuachwa nyuma kimasomo na wenzao wa kike jambo ambalo alisema lisiachwe kama lilivyo na likaonekana la kawaida.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benjamin Mkapa Fundation, Dk. Ellen Senkoro, alisema wamejadili namna teknolojia inavyoweza kurahisisha utoaji wa huduma za afya na kufuatilia hali za wagonjwa.

"Tumesikiliza ubunifu mbalimbali wa wahitimu wa chuo hiki na wale waliohitimu miaka ya karibuni. Kwa kweli ubunifu unavutia sana na kazi ambazo wanafanya kidijitali zinatia moyo. Kwa hiyo nawahimiza madaktari watakaohitimu wawe wabunifu ili huduma hizi zitolewe kidijitali," alisema.

Dk. Senkoro alisema kwa kuwa umeme si tatizo tena nchini ni rahisi madaktari hao wakabuni mifumo ambayo itawaitumia kuhudumia wagonjwa wao kwa kuwa Watanzania wengi wanasimu janja.

"Mabadiliko duniani yanakwenda kwa kasi kwa hiyo lazima tuwe wabunifu. Ifikie wakati si lazima sana kwenda hospitalini au kituo cha afya. Unaweza ukafanya vipimo ukiwa nyumbani na ukapata majibu yako kwa kutumia simu yako ya mkononi," alisema.

Alisema amefurahishwa kuona tuzo nyingi zilizotolewa kwenye kongamano hilo zimechukuliwa na wahitimu wa kike na kwamba hali hiyo inaonyesha kuwa kuanzia mfumo wa sekondari wanafunzi hao wameandaliwa vizuri.

"Mafanikio haya yanaonyesha kuwa wanawake tunaweza kushika nafasi mbalimbali za uongozi tofauti na mitazamo iliyokuwa zamani na hivi sasa tuna kazi kubwa ya kuhakikisha tunawawezesha watoto wa kiume kujua kwa nini wanarudi nyuma ili tuweke uwiano," alisema.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Kairuki, Prof. Yohana Mashalla, alisema kongamano la mwaka huu lilikuwa mahususi kwa ajili ya kujadili matumizi ya dijitali katika kufanikisha utoaji wa huduma za afya kwa urahisi nchini.

"Tumejiuliza dijitali ipo watumiaji wapo, je gharama zake zikoje na halafu kwa sababu ziko nyingi ni ipi gharama yake tunaweza kuimudu kuinunua kwa mazingira ya hapa nchini.

"Hizi teknolojia zinakuja na zinabadilika mara kwa mara tunapaswa kujiuliza je tuna wataalamu au vyuo vya kutosha vitakavyofundisha namna ya kutumia teknolojia hizo na zinavyotumika kwa usahihi," alisema.




Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Christopher Newton, akitoa elimu kuhusu ukatili wa kijinsia, wakati wa maadhimisho ya Siku 16 Kupinga Ukatili Kijinsia yaliyoandaliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, katika viwanja vya Kawe, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Upasuaji wa kurejeleza viungo vilivyokakamaa waleta kicheko

**Na Beatrice Shayo**

JUMLA ya wanawake na wasichana 27 wamefanyiwa upasuaji wa kurejesha uwezo wa kutembea na kukunjua viungo vilivyokakamaa ambao walipata ulemavu kutokana na majeraha ya moto, ukatili wa kijinsia na ajali.

Daktari Bingwa wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuaji katika Hospitali ya Aga Khan, Dk. Athari Ali, aliwaambia waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuwa mpango huo unalenga kurejesha uwezo wa kimwili ili kuleta nguvu na kuboresha ubora wa maisha ya wanawake na wasichana.

Alisema Novemba 29 hadi Desemba 6, mwaka huu, hospitali hiyo kwa kushirikiana na asasi Reconstructing Women International (RWI) na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), imefanya upasuaji wa kurekebisha maumbile katika awamu ya tisa ya programu hiyo endelevu iliyoanzishwa mwaka 2016.

Dk. Ali alisema katika awamu tisa zilizopita kati ya mwaka 2016 hadi mwaka 2023, zaidi ya wagonjwa 300 wamenufaika na upasuaji huo wa bure. Pia madaktari 16 wa upasuaji wa kurekebisha maumbile, upasuaji wa jumla na wanafunzi wa tiba kutoka hospitali mbalimbali za umma na binafsi wamepata mafunzo kupitia mpango huo.

Alisema madaktari hao wengi ni wa ndani na sasa wanaweza kutoa upasuaji wa kurekebisha mwili katika hospitali za umma.

"Kutokana na wingi wa wagonjwa hawa nchini taasisi ya huduma za afya ya Aga Khan na washirika wake, wanakusudia kupanua kambi za mpango huu kutoka mara moja hadi mara mbili kwa mwaka," alisema Dk. Ali.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Kurekebisha Mwili kutoka MNH, Edwin Mrema, alisema kadri idadi ya watu nchini inavyoongezeka mahitaji ya huduma maalumu za afya, ikiwa ni pamoja na upasuaji wa kurekebisha mwili yanaongezeka.

Alisema ili kukabiliana na suala hilo, serikali inashirikiana na Muhimbili na mashirika ya kimataifa ikiwamo RWI.

"Ushirikiano huu unalenga kujenga uwezo wa madaktari wa ndani, kuboresha upatikanaji wa vifaa vya kisasa na kuleta madaktari wataalamu kutoka nje ya nchi," alisema.

Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Kurekebisha Mwili ambaye ni kiongozi wa timu ya RWI, Andrea Pusic, alisema wamekuwa na uwezo wa kutoa huduma wa wanawake na wasichana wengi waliokumbwa na majeraha, ili kuboresha uwezo wao wa kimwili na muonekano mzuri.

Naye Daktari Bingwa wa Upasuaji kwa Matundu Madogo katika Hospitali ya Aga Khan, Aidan Njau, alisema wagongwa hao huwapata mikoani na kuangalia walioumia kwa kiwango kikubwa ili kuwapatia huduma hiyo ya upasuaji kwa kuwarejeshea tumaini na tabasamu kwa wanawake na wasichana wa Tanzania.

"Yuko mwanamke ambaye titi lake lilisagika. Huyu tulimfanyia upasuaji na kwa sasa yuko katika hali nzuri. Alikosa matumaini ya kupona na wengine waliopata majeraha makubwa kutokana na ajali za gari hali iliyowasababishia kupata ulemavu wamepona," alisema Dk. Njau.

Alisema programu hiyo hufanyika kila mwaka na madaktari maalum kutoka Ulaya na Marekani hutoa huduma na mwitikio kwa wananchi ni mkubwa.

Dk Njau alisema matibabu yanayotolewa huwa ni gharama kubwa lakini wanayatoa bure kwa wananchi, hivyo Watanzania wachangamkie fursa hiyo ya matibabu.

HABARI KITAIFA

# Watu 97 watiwa mbaroni, wamo wa mauaji, ubakaji

**Na Grace Mwakalinga**

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya limewakamata watu 97 kwa tuhuma mbalimbali zikiwamo mauaji, kujeruhi, kumiliki silaha kinyume cha sheria, kupatikana na dawa za kulevya na kuingia nchini bila kibali.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Benjamin Kuzaga, alithibitisha jana kuwa watu hao hao walikamatwa Novemba, mwaka huu, baada ya kuimarisha ulinzi katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema operesheni hizo zililenga kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu ili wananchi waendelee na shughuli za kujipatia kipato halali bila usumbufu.

Katika operesheni iliyofanyika Novemba 21, mwaka huu, katika kijiji cha Igawa wilayani Mbarali, alisema watu wanne walikamatwa wakiwa na dawa za kulevya aina ya bangi.

Alisema Shamim Maxwell (37) na Itika Bugale (36) wakazi wa Uyole, walinaswa wakiwa na kilo 33.5 za bangi ndani ya mabegi mawili katika basi la Kampuni ya Achimwene lililokuwa likienda Dar es Salaam.

SACP Kuzaga alisema kondakta wa basi la Abood, Erick Mathew (46), na utingo wake, Stanslaus Nyagawa, walikamatwa wakiwa na kilo 20 za bangi zilizohifadhiwa katika mifuko ya sandarusi, wakisafirisha kutoka Songwe kwenda Dar es Salaam.

Katika tukio lingine, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na askari wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), limemkamata Adam Katani (58) kwa tuhuma za kumiliki silaha aina ya gobore, vipande 30 vya chuma vinavyotumika kama risasi, unga wa baruti na vipande vya nyama ya pimbi.

Kamanda Kuzaga alisema mtuhumiwa huyo alikuwa akijihusisha na uwindaji haramu katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Katika hatua za kisheria, Kamanda Kuzaga alithibitisha kuwa kesi kadhaa zimepata mafanikio, zikiwamo za ubakaji.

Alisema Erick Simtengu (24) amehukumiwa kifungo cha miaka 30 kwa kumbaka mwanafunzi wa kidato cha pili na Modrick Elias Mwakibete (21) amehukumiwa kifungo cha miaka 30 kwa kumbaka mtu mzima baada ya kumtishia kwa kisu.

Katika kesi ya mauaji, Kamanda huyo alisema Emanuel Mwesya (24) na David Mwalindu (25) wamehukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua Lufingo Asumwisye (37) na kuiba pikipiki yake.

Kamanda Kuzaga alisema makosa ya usalama barabarani 10,580 yameredkodiwa Novemba, mwaka huu, na madereva wawili walifungiwa leseni, huku kesi saba za usalama barabarani zikifikishwa mahakamani na kumalizika kwa mafanikio.

# Taasisi zaungana kuboresha huduma za afya

**Na Mwandishi Wetu**

JUKWAA la kibunifu la Utalii wa Matibabu la Afrika Kusini na American Clinic, wanatarajia kushirikiana kuboresha upatikanaji wa huduma za afya na uvumbuzi katika Sekta ya Afya Afrika, yakiwamo magonjwa ya saratani na moyo.

Ushirikiano huo unalenga kusaidia wagonjwa kwa kuunganishwa na madaktari bingwa na wataalamu ili kuwapatia wagonjwa huduma za kidijitali na kuboresha utoaji huduma za afya baina ya nchi za Afrika, ikianza na Tanzania na Afrika ya Kusini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Najali Care, Dk. Nandipha Ndhlovu, alisema jana Dar es Salaam kuwa lengo ni kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa wagonjwa na kujenga mifumo ya afya ya kidijitali Alisema ushirikiano huo ni hatua muhimu kuelekea kuboresha huduma za afya pale mgonjwa anapohitaji msaada nje ya mipaka ya nchi yake.

"Tunahakikisha wagonjwa wanapata msaada wa kina kuanzia ushauri wa huduma inayostahili kutolewa kabla ya matibabu kuanza, mipango ya safari hadi huduma za ufuatiliaji wakati na baada ya matibabu," alisema.

Alisema ushirikiano huo unaimarisha mifumo ya afya baina ya nchi hizi mbili, kupitia kubadilishana maarifa na kujengeana uwezo, na hivyo kuimarisha nafasi ya Afrika katika ubunifu wa huduma za afya duniani.


"Ushirikiano huu unawapa wagonjwa huduma mbalimbali, ikiwamo ushauri wa awali ya matibabu, usafiri uliorattibiwa na malazi na upatikanaji wa matibabu maalum Afrika Kusini.

"Wagonjwa pia, watanufaika na huduma za ufuatiliaji baada ya matibabu kabla ya kurejea nchini, na pale wanaporudi kuhakikisha mwendelezo wa huduma," alisema.

Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Hospitali ya American Clinic, Violet Luwanja, alisema ushirikiano huo unakamilisha jitihada za serikali ya Tanzania za kuboresha utoaji wa huduma za afya na kupanua upatikanaji wa huduma bora.

Alisema afya ya kinga ni msingi mwingine wa ushirikiano huo, kupitia kampeni za afya za kijamii na mipango ya kuwezesha wagonjwa kugundua mapema magonjwa ya muda mrefu, kama saratani na magonjwa ya moyo.

Soko la utalii wa matibabu linakadiriwa kuwa dola bilioni 180 duniani kufikia mwaka 2026.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia), Shekhe Mkuu wa Tanzania, Mufti Abubakar Zuberi (watatu kushoto) na Shekhe Mkuu wa Zanzibar, Salehe Omar Kabi (wanne kushoto), wakionyesha sehemu ya vitabu 3,000 vya elimu ya dini, Dar es Salaam juzi, ambavyo serikali imelipatia Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), kwaajili ya kusambazwa katika shule binafsi. **PICHA MAULID MMBAGA**

# Othman: Hakuna kuchoka wala kukata tamaa kupigania mageuzi

**Na Mwandishi Wetu**

Mwenyekiti wa Chama cha ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, amewataka wananchi wa Zanzibar kutochoka wala kukata tamaa katika kupambania mageuzi ya kisiasa na kiuchumi.

Othman aliyasema hayo jana Chaleni Muambe, jimbo la Kiwani wilaya ya Mkoani na Mbuzini Jimbo la Ziwani Mkoa wa kusini Pemba alipowasalimia wananchi na wafuasi wa chama hicho baada ya kumaliza kuwasajili wanachama wapya katika mfumo wa ACT Kiganjani.

Pia alisema ni lazima wananchi waungane katika jitihada za kufanikisha malengo ya chama ya kuleta mageuzi ya kuwasaidia Wazanzibari kupata Zanzibar mpya itakayokuwa na mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kimaendeleo, ambalo ndilo lengo la chama hicho.

Othman ambaye pia ni Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, alisema Zanzibar imejaliwa neema nyingi na rasilimali muhimu za kiuchumi, hivyo kinachohitajika ni nguvu za pamoja katika kuwapata viongozi bora wenye maono na nia ya kweli ya kutetea wananchi sambamba na kuleta maendeleo.

Kwa mujbu wa taarifa iliyotolewa ma Kitengo cha Habari Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman alisema hakuna taifa lolote duniani linaloweza kupiga hatua kwa kutegemea mikopo kutoka nje au misaada kutoka kwa wahisani.

Alisema jambo muhimu ni kuzitumia rasilimali zilizopo ili zitumike vyema chini ya viongozi waadilifu wenye uwezo wa kukuza uchumi na maendeleo ya Zanzibar.

Pia alisema Zanzibar ni nchi yenye sifa njema nyingi na kupendwa na kila mtu kutoka sehemu mbalimbali duniani hasa kwa kuzingatia mahali ilipo kibiashara kulingan isha na yalivyo mataifa mengine duniani.

Alisema serikali ni kawaida yake kwamba haifanyi biashara badala yake ni mkusanyaji wa mapato sambamba na kuwa na mamlaka yake katika kuvitumia vyanzo muhimu vya kiuchumi katika kusaidia nchi yake.

Kuhusu usajili wa wanachama katika mfumo wa ACT Kiganjani, alisema suala hilo ni utekelezi wa takwa chama linalowataka viongozi wote wakuu kushiriki katika kuwasajili wanachama kwenye mfumo huo ili kutimiza malengo ya chama ya kuwa na mtaji mkubwa wa wanachama watakaokiletea ushindi chama hicho.

Sambamba na hilo, alisema kuwapo mambo 40 yaliyoingizwa kwenye orodha ya Muungano kunainyima Zanzibar mamlaka katika kuendeleza jitihada za kukuza uchumi wake ambao kwa muda mrefu umewafanya wananchi kuendelea kuwa na maisha duni. Naibu Katibu Mkuu wa ACT- Wazalendo Zanzibar, Omar Ali Shehe, alisema ziara za mwenyekiti na kazi ya kuwasajili wanachama anayoifanya yeye mwenyewe inakumbusha viongozi jukumu la kuwa chini na wananchi kuendeleza masuala mbalimbali.

Othman katika ziara hizo amesajili wanachama 438 na leo anendelea na ziara ya kichama na anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika kongamano la wanawake wa ACT Wazalendo litakalofanyika katika ukumbi wa Sameili, Gombani Chake Chake, kisiwani Pemba.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga, ushindi wa ugenini CAF unawezekana

**MASHINDANO** ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka chini ya usimamizi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho sasa yako katika hatua za makundi.

Awali Tanzania Bara ilikuwa inawakilishwa na timu nne katika mashindano hayo, mabingwa wa Ligi Kuu, Yanga na Azam FC wakishiriki katika michuano ya Ligi ya Mabingwa huku Simba na Coastal Union zenyewe zikipeperusha bendera ya nchi kwenye mashindano Kombe la Shirikisho.

Kwa upande wa Visiwani Zanzibar, JKU SC ilikuwa inachuana katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa huku Chipukizi ya Pemba walikuwa wanapambana kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho baada ya kuibuka mabingwa wa Kombe la ZFF Cup ( Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar).

Kwa sasa ni timu mbili tu ndio zimebakia katika mashindano hayo ambazo ni Yanga na Simba zote za Dar es Salaam.

Katika hatua ya makundi, Yanga iliyoko chini ya Kocha Mkuu, Sead Ramovic, imepangwa Kundi A pamoja na Al Hilal ya Sudan, TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo) na MC Algers ya Algeria huku Simba ikiwa na Bravos do Maquis ya Angola, CS Constantine ya Algeria na CS Sfaxien ya Tunisia.

Yanga ilianza hatua hiyo kwa kufungwa mabao 2-0 na Al Hilal, ikicheza nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa wakati Simba ikiwa kwenye dimba hilo hilo ilipata ushindi wa goli 1-0.

Ratiba ya michuano hiyo inaonyesha wawakilishi hao wawili wote wikendi hii watakuwa Algeria kusaka pointi muhimu ili kujiimarisha katika msimamo na kujiweka kwenye mazingira chanya ya kusonga mbele.

Yanga wao leo watashuka kuwakabili MC Alger ambayo katika mechi yake ya kwanza iligawana pointi na TP Mazembe, mechi iliyofanyika mjini Lubumbashi huku kesho Wekundu wa Msimbazi wali-yowafuata CS Constantine watachuana kuhakikisha wanaondoka na pointi za ugenini. Tunaamini maandalizi mazuri ambayo yalifanywa na timu hizi mbili kuanzia kusajili wachezaji wenye ubora unaofanana na ukubwa wa mashindano hayo ya CAF watahakikisha wanalinda heshima ya klabu wanazotoka kwa kupata ushindi.

Wachezaji ambao watafuata vyema ushauri wa benchi la ufundi, watakuwa na nafasi kubwa ya kufanya vizuri katika mechi ya leo na kesho na kuwapa furaha mashabiki wake, lakini pia kuipa heshima nchi iliyoko chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Miaka ya nyuma ilikuwa ni nadra sana kuona timu inapata ushindi ugenini, lakini dunia ya sasa imebadilika, Simba, Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), zimekuwa zikivuna matokeo bora ugenini.

Kwa misingi hiyo, huu ni wakati mwingine kwa wachezaji, viongozi na wadau wa timu hizo mbili kuhakikisha wanajiweka kwenye mazingira rafiki ambayo yatasaidia kuondoka na ushindi katika mechi hizo za ugenini.

Utulivu na umakini unatakiwa kuongezeka, kila mchezaji anatakiwa kufahamu jukumu lake ni kuhakikisha bendera ya klabu na Tanzania inapeperushwa vyema kwa kucheza katika kiwango cha juu, lakini wakumbuke ubora watakaoonyesha utawasaidia kupandisha thamani yao.


Hatua ya makundi ya michuano ya CAF, huvutia mawakala na makocha mbalimbali, hivyo kufanya vizuri kwa timu na mchezaji, ni daraja la kuelekea kucheza soka nje ya Afrika, wakumbuke ukiondoa Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON), michuano hii ya ngazi ya klabu hutoa nafasi kwa wachezaji wengi zaidi 'kujiuza sokoni'.

Kwa maslahi ya nchi, huu si wakati wa kuombeana dua mbaya, kila upande uhakikishe unajiimarisha katika kusaka ushindi na ushindani wao utarejea watakapokutana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hakuna kinachoshindikana, kuvuna pointi tatu au moja ugenini inawezekana.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Simba, Yanga zicheze kwa nidhamu, heshima Algeria

**WAWAKILISHI** wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa, Simba na Yanga leo na kesho zitashuka ugenini Algeria kwenye miji tofauti kwa ajili ya kusaka pointi tatu muhimu.

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga leo hii kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za Tanzania watashuka kwenye jiji la Algiers kucheza mechi ya pili ya Ligi ya Mabingwa hatua ya makundi dhidi ya MC Algers.

Utakuwa mchezo wa raundi ya pili wa Kundi A, ambapo Yanga itakuwa na kazi moja ya kuhakikisha haipotezi mechi hiyo baada ya kufungwa mabao 2-0 katika mchezo wa raundi ya kwanza dhidi ya Al Hilal ya Sudan.

Simba ambyo ipo kwenye Kundi A, Kombe la Shirikisho Afrika, nayo itateremka kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui kwenye mji wa Constantine kesho kucheza dhidi ya CS Constantine.

Utakuwa ni mchezo wa pili kwa wawakilishi hao wa Tanzania, baada ya kushinda bao 1-0 nyumbani dhidi ya Bravo do Maquis.

Hii ni michezo muhimu sana kwa wawakilishi wote wa Tanzania katika azma ya kuona zote zinapita kwenye hatua hii ya makundi na kwenda robo fainali.

Hata hivyo, ukweli lazima usemwe hazitakuwa mechi rahisi kwenye makaratasi, badala yake itabidi mabenchi ya ufundi na wachezaji wafanye kazi ya ziada.

Inahitajika machozi, jasho na damu ili kuhakikisha timu hizo zinapata pointi tatu au moja katika michezo yao nchini Algeria.

Nasema hivi kwa sababu najua timu za Kusini mwa Jangwa la Sahara zinapokwenda kucheza mechi na timu zilizo nchi za Afrika Kaskazini zilizozungukwa na bahari ya Mediterania. Huku nchini mashabiki wa soka huziita timu za 'Kiarabu.'

Mara nyingi hupata tabu kwa kila kitu kuanzia nje ya uwanja mpaka ndani, yaani wakati mwingine tabu huanzia pale zinaposhuka uwanja wa ndege, hotelini, sekeseke la mashabiki uwanjani, na upinzani mkali ndani ya uwanja.

Timu za Afrika Kaskazini zina aina yao ya mpira ambayo ni ya kumiliki sana mpira, zikicheza kwa kasi, zikipenda zaidi kutumia mawinga, kushambulia hasa zikicheza kwao.

Mara nyingi huzipa tabu timu za Afrika zilizo chini ya Jangwa la Sahara, ambazo hutumia zaidi mifumo, plani za makocha na vipaji binafsi vya wachezaji, lakini hazijajaliwa kasi.

Pamoja na kwamba timu za Simba na Yanga zimeshawahi kupambana na timu kubwa za Afrika kama Al Ahly ya Misri, Wydad Casablanca, Raja Casablaca za Morocco, Al Ahli Tripoli ya Libya, Club Africain ya Tunisia na nyingine nyingi, lakini isizidharau timu hizi kwa sababu hazina majina makubwa.

Kwa kiasi kikubwa aina ya uchezaji wao inafanana na hata wachezaji wao wanakuwa na wale wale, anatoka huku anakwenda kule, hivyo Simba na Yanga isizichukulie poa kwani zinakuwa hatari sana zinapocheza nyumbani kwao.

Timu za Kiarabu unaweza kuziona kama nyanya zinapocheza ugenini, lakini zikishakuwa nyumbani zinakuwa kitu tofauti kabisa.

Cha kufanya kwa timu za Tanzania si kwenda kujiachia kama zinacheza mechi za Ligi Kuu. Badala yake zicheze kwa tahadhari sana, ziache mianya, kwani kiasili wachezaji wa Kaskazini wana vipaji wakiwa na mpira miguuni na kushambulia mianya inayopatikana.

Kinachotakiwa ni kucheza kwa nidhamu na kuwaheshimu wenyeji ambao watakuwa wakisaidia na hali ya hewa waliyoizoea.

Simba na Yanga zinatakiwa kucheza kwa tahadhari, kuzuia zaidi na kushambulia kwa kushtukiza, wakirudi kukaba pamoja kama hawana mpira. Hii itazisaidia sana kama si kupata pointi tatu basi hata moja.

Kitendo cha kutaka kupishana na wachezaji wenye kasi ambao hali ya hewa ya baridi inawasaidia na kuwaathiri wawakilishi wetu kinaweza kusababisha madhara kwenye matokeo ya mchezo.

Nawatakia kila la heri katika michezo yao nchini Algeria.

# Mwinyi aahidi Zanzibar kuwa kituo cha utalii usio wa msimu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema inakusudia kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikubwa cha utalii wa kisasa usio na misimu kwa kuwavutia wawekezaji na wageni wengi.

Imesema Zanzibar bado inawakaribisha wawekezaji zaidi kwa kuwa ina maeneo mengi ambayo hayajafikiwa kwa fursa nyingi za uwekezaji.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo juzi Ikulu - Zanzibar alipozungumza na Balozi mpya wa Uingereza nchini Tanzania, Marianne Young, alipofika kujitambulisha.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Mawasiliano, Ikulu Zanzibar ilibainisha kuwa Dk. Mwinyi alisema bado Zanzibar ina uhitaji mkubwa wa uwekezaji kwenye sekta ya Uchumi wa Buluu kupitia utalii, bandari, mafuta na gesi pamoja na usafirishaji wa majini.

Alisema kwa muda mrefu Zanzibar imekuwa ikitangaza utalii wa zamani wa urithi ukiwamo wa Mji Mkongwe wa Zanzibar na fukwe, hivyo akasema wakati umefika Zanzibar kuendelea kujitangaza pia na utalii wa kisasa ukiwamo utalii wa mikutano ya kimataifa, michezo.

Taarifa hiyo ilisema Rais mwinyi alitolea mfano michezo ya mbio za magari ambazo zimekuwa kivutio kikubwa duniani na kuwavutia mashabiki na wageni wengi maarufu kama Formula One.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi amesema dhamira ya serikali ni kuwa na utalii wa hadhi ya juu utakaowavutia wageni wengi bila kujali misimu ya utalii. Pia alisema nchi imejiandaa kuwa na misimu yote ya utalii kwa kuimarisha vivutio zaidi vyenye kuwavutia wageni wengi.

Kuhusu ongezeko la utalii, Dk. Mwinyi alieleza dhamira ya serikali kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara na mawasiliano vikiwamo viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba kuemdelea kuwa na hadhi ya kimataifa.

Dk. Mwinyi pia alizungumzia fursa za bandari jumuishi kwa Zanzibar ambayo serikali imewekeza nguvu kubwa Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja alikoeleza kwa sasa Zanzibar inahitaji bandari kubwa ili kukidhi mahitaji ya uchumi kama kituo muhimu cha usafirishaji, usambazaji wa bidhaa, kutoa huduma na kufanyia biashara ikiwamo kupokelea mizigo, kusafirishia mazao na mahitaji mbalimbali kama mafuta, nafaka, na kukuza Uchumi.

Pia aligusia suala la mafuta na gesi pamoja na usafiri wa majini, akieleza Zanzibar inavyohitaji uwekezaji mkubwa kwenye sekta hiyo na kuiomba serikali ya Uengereza kuangalia uwezekano wa kuunga mkono.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi amewakaribisha wawekezaji zaidi wa Uingereza Zanzibar kwa wingi kuwekeza na kunufaika na fursa za uwekezaji zilizopo.

Balozi Young alimhakikishia Rais Dk. Mwinyi kuwa serikali ya Uingereza itaendelea kuunga mkono Zanzibar kuimarisha ustawi wa kuleta maendeleo hasa katika masuala ya afya, elimu na Uchumi wa Buluu.

Alisema utalii ni fursa muhimu baina Zanzibar na Uingereza katika kuimarisha ushirikiano wa pande mbili na kuiahidi Zanzibar kushirikiana kiufundi kwa uzoefu kwa masuala mbalimbali ya Uchumi, jamii na teknolojia.

Pia Balozi Young alisifu juhudi za SMZ kwa maendeleo makubwa iliyofikiwa hasa kwa sekta ya mawasilino na miundombinu.

Balozi Young akiteuliwa kuwa Balozi wa Uingereza nchini Tanzania Agosti, mwaka huu.




Askari mgambo ambaye ni mlinzi wa Kituo cha Bajaji cha Kitunda, jijini Dar es Salaam, akiifunga moja ya bajaji iliyokuwa imeegeshwa kwa kukiuka taratibu katika kituo hicho, juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kocha Simba aeleza alivyoteswa na maofisa wa DCEA

**Na Grace Gurisha**

MMILIKI wa Kituo cha Cambiasso Sports Academy, Kambi Zuberi Seif na aliyekuwa kocha wa makipa wa timu ya Simba, Muharami Sultan, wameieleza mahakama kuwa walikiri kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya kutokana na mateso waliyopewa, ikiwamo kuvuliwa nguo zote na kuning'inizwa juu.

Aidha, wamedai kuwa hata walipofikishwa mbele ya mlinzi wa amani katika Mahakama za Mwanzo, walilazimishwa kutia saini maelezo ambayo hawakuyatoa, na kutishiwa kuwa wasipotia saini wangeuawa.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroin ambao nao waliteswa kukiri mashtaka hayo ni Maulid Mzungu, maarufu kama Mbonde, Said Matwiko, Fundi Selemara na John Andrew, maarufu kama Chipanda mfanyakazi wa Cambiasso.

Pia mshtakiwa wa sita katika kesi hiyo, Sara Joseph ambae ni mke wa Said, alidai kuwa tangu akamatwe mwaka 2022, hakuwahi kutia Saini nyaraka yoyote.

Washtakiwa hao walidai hayo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Aaron Lyamuya wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, baada ya kumaliza kusomewa maelezo ya mashihidi Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, akisaidiana na Roida Mwakamele.

Hakimu Lyamuya aliwauliza washtakiwa kama wanachochote cha kuzungumza kama kanuni inavyotaka ndipo wakili wa mshtakiwa Kambi, Dominicus Nkwera, alipodai kuwa shahidi namba mbili na tatu ni mtu mmoja ambaye ni Innocent Masangula.

"Tunaomba iingie kwenye rekodi kwamba huyu shahidi ni mtu mmoja lakini ana maelezo mawili tofauti na tarehe tofauti," alidai Wakili Nkwera.

Pia alidai kuwa iingie kwenye rekodi kwamba mteja wake, Kambi, baada ya kukamatwa aliteswa sana na maofisa polisi wa DCEA na kudhalilishwa utu wake ili akubali kutia saini nyaraka.

"Kulingana na mateso aliona bora atie saini nyaraka za kukiri kosa kuokoa maisha yake na hata alipopelekwa kwa mlinzi wa amani, walimtishia kwamba asipotia saini maelezo atakayoyakuta huko akirudi tena polisi mateso yataendelea kawa kawaida," alidai.

Mshtakiwa wa pili, Sultan, alidai kuwa alipigwa sana na kudhalilishwa mbele ya wanawake, akilazimishws kutia saini vitu ambavyo hakuvielewa na hata mlinzi wa amani aliona makovu aliyokuwa nayo mwilini.

"Nimakuuliza mlinzi wa amani kwamba narudi kule kule nilikotoka akasema ndiyo, sheria ndiyo inaelekeza hiyo, nikamwambia nikirudi wataniua," alidai Sultan.

Pia mshtakiwa Chipanda alidai kuwa alipigwa sana na akalazimishwa kutia saini maelezo.

Mshtakiwa wa nne, Said, alidai kuwa akiwa Kituo cha Polisi alilazimishwa kutia saini karatasi ambazo hazijui na Novemba 21, 2024 alisainishwa karatasi zingine Kisutu, hayo yote zilikuwa na ahadi za maofisa wa DCEA kuwa ni akikiri watamwachia mke wake, Sara.

Mshtakiwa wa tano, Maulid, aliieleza mahakama akiwa kituoni alisainishwa maelezo ambayo hayajui na pia waliteweza utu wake, wakamvua nguo na wakamning'niza kwenye bomba, wakamweleza kwamba hawaoni hasara taifa likipoteza mtu mmoja.

Alidai kuwa kwa mlinzi wa amani hakuzungumza wanayoyataka wao.

Mshtakiwa Sara alidai walimchukua mume wake nyumbani wakaondoka naye baadaye walimfuata yeye wakamchukua na tangu kipindi hicho hajawahi kutia saini karatasi yoyote.


Washtakiwa walidai kuwa katika utetezi wao watakuwa na mashahidi na baadhi yao walidai watakuwa na vielelezo.

Kesi hiyo itatajwa Februari 10,2025 Mahakama Kuu.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa Oktoba 27, 2022 wakiwa Kivule, Ilala mkoani Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroin kilogramu 27.10.

Katika shtaka la pili ilidaiwa kwamba Novemba 4, 2022, eneo la Kamegele, Mkuranga mkoani Pwani, kwa pamoja walikutwa wakisafirisha kilogramu 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroin.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wahimiza uzalishaji bidhaa zenye ubora kimataifa

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imeahidi kutilia mkazo uzalishaji wa bidhaa zenye ubora wa kimataifa ili kuongeza ushindani katika soko la dunia na kukuza uchumi na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Selemani Jafo, alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam, wakati wa Maadhimisho ya Kimataifa ya Siku ya Ushindani Duniani 2024, yaliyoandaliwa na Tume ya Ushindani (FCC).

Maadhimisho hayo yalifanyika sambamba na kongamano lililohusisha wadau wa FCC, wajasiriamali wa bidhaa mbalimbali na wanafunzi wa vyuo vikuu, kujadili namna ya kufikia fursa za ajira kwa kuzalisha bidhaa zenye ubora wa kimataifa.

Jafo aliwataka vijana kuchangamkia fursa ya masoko ya nje ya nchi kwa kuwa serikali imeshatengeneza mazingira na kufungua masoko mataifa mbalimbali duniani.

Alitoa mfano kuwa, Tanzania inauza bidhaa nje ya nchi zenye thamani ya Dola milioni 85 pekee, wakati mataifa mengine yakiwa yamefikia kuuza bidhaa za hadi Dola bilioni 2.

"Hii ni fursa kubwa kwetu Watanzania kuendelea kuchangamka kwa kuzalisha bidhaa zitakazo shindanishwa kimataifa, "alisisitiza Jafo.

Alisema serikali imeshaweka mazingira wezeshi ya kuzalisha bidhaa zenye ubora kupitia ujenzi wa miradi ya mikakati kama Reli ya Kisasa (SGR) na ujenzi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Nyerere, hivyo jukumu limebaki kwa wajasiriamali na vijana.

Aidha, alitaka Watanzania kuendelea kuitunza miradi ya iliyoanzishwa na serikali ili kuweka ushindani na mataifa mengine duniani.

Jafo aliomba kupata mrejesho wa changamoto zitakazojadiliwa katika kongamano hilo, ili serikali izifanyie kazi na kupata suluhu ya kudumu.

Mwenyekiti wa Bodi ya FCC, Dk. Aggrey Mlimuka, alisema maadhimisho hayo ambayo hufanyika kila mwaka Desemba 5, kwa mwaka huu yameangazia namna sera na sheria za ushindani zinavyotumika kupunguza kukosekana kwa usawa katika uchumi.

Alisema lengo ni kuhakikisha sera na sheria zote zinakuwa katika usawa wa kuleta ushindani sawa katika kuuza na kununua bidhaa na kutoa huduma kwenye soko bila kuwapo na vikwazo. Alisema FCC imejipanga kutoa huduma bora kwa wateja, wadau na kusimamia vyema soko la Tanzania Bara, ili kuondoa kukosekana kwa usawa wa bidhaa zinazoingia sokoni.

# Wafanyabiashara Kariakoo waona nuru mpya

**Na Pilly Kigome**

BAADHI ya wafanyabiashara wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Kariakoo (JWK) wamesema wanaiona Kariakoo mpya ijayo baada ya kupata viongozi wapya.

Wamesema viongozi waliopatikana jana katika uchaguzi mkuu, ni makini, wasomi na waadilifu na hivyo kujiona wanakwenda katika mafanikio makubwa ya kibiashara ndani na nje ya nchi.

Wamesema viongozi hao ambao wataongoza katika kipindi cha miaka mitatu hadi mwaka 2027, wanaamini watawasikiliza na kuwaunganisha kwa sababu wamechoshwa na viongozi viburi walioshindwa majukumu yao na waliojiingiza katika siasa.

Nafasi zilizokuwa zinagombaniwa katika uchaguzi huo ni za mwenyekiti, makamu mwenyekiti, katibu, naibu katibu, mhazini na wajumbe 15.

Idadi ya wajumbe waliotakiwa kupiga kura ni 448 na aliyeibuka kidedea katika nafasi ya uenyekiti ni Serini Mushi, aliyepata kura 229 na kufuatiwa na Fedrick Lutindi aliyepata kura 160 na Martin Mbwana aliyekuwa akitetea nafasi hiyo kupata kura 12.

Nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilichukuliwa na Mfaume Mfaume, aliyepata kura 251 na nafasi ya Katibu imechukuliwa na Renutus Mlerwa aliyepata kura 204. Nafasi ya Mhazini imekwenda kwa Enock Lampard aliyepata kura 264.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi huo, Richard Kijogoo, alisema umefanyika kwa haki na usalama mkubwa.

Alisema kamati hiyo imefanya kazi kubwa hadi uchaguzi huo kufanyika bila kasoro na kukosekana kwa uvunjifu wowote wa amani.

Mwenyekiti mpya, Mushi, alisema jukumu lake kubwa ni kuhakikisha anaileta Kariakoo mpya isiyokuwa na migogoro na migomo.

"Naamini na wameniamini kwa kiasi kikubwa na nitakwenda kuwapigania wafanyabiashara kwa nguvu kubwa na kuunganisha wafanyabiashara wote na kuahidi kufanya kazi kwa weledi kwa ushirikiano mkubwa na serikali" alisema.

Mishi alisema ataunda chombo ambacho kitasaidia kutoa ushauri kwa Tume ya Rais Maboresho ya Kodi iliyoundwa Oktoba, mwaka huu.




Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mwafatma Mohamed (kulia), akikabidhi cheti kwa baadhi ya wanafunzi walionufaika na mradi wa TEHAMA na programu ya 'Skills for their Future' kutoka shule za sekondari za Karinuni, Miburani na Wailes, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Shule Dar zanufaika mradi wa TEHAMA

**Na Joseph Mwendapole**

SHULE tatu za wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, zimenufaika na mafunzo ya kuendeleza ujuzi yajulikanayo kama "Skills for their Future" kupitia mradi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

Mradi huo umefadhiliwa na shirika lisilo la kiserikali la BRAC Maendeleo Tanzania kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu wa Taifa unaosimamiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA).

BRAC - Maendeleo Tanzania kwa kushirikiana na TEA, imetekeleza program hiyo kwa miaka mitatu katika shule za sekondari za Karibuni, Miburani na Wailes katika Manispaa ya Temeke. Mradi huo ulianza mwaka 2022 na hadi inafikia ukomo Desemba, mwakah uu, imenufaisha wanafunzi 1,922 na walimu 64.

Akizungumza juzi katika hafla ya kufunga programu hiyo, iliyokuwa ikitoa mafunzo ya kidigitali kwa vijana katika shule hizo, Kaimu Meneja Usimamizi Miradi ya Elimu wa TEA, Mwafatma Mohamed, alisema programu hiyo ni ya kipekee katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Alisema TEA inajivunia ushirikiano na BRAC Maendeleo Tanzania katika juhudi za kuboresha elimu na maendeleo ya taifa.

Mwaka 2022, alisema TEA ilitia saini makubaliano maalum ya ushirikiano na BRAC - Maendeleo Tanzania ambayo ni mdau muhimu wa maendeleo katika Sekta ya Elimu hapa nchini.

Alisema kupitia ushirikiano huo, kompyuta 60 na vishkwambi 60 vyote vyenye thamani ya Sh. milioni 132.6 vilitolewa kwenye shule tatu za sekondari wilayani Temeke.

Pia aliipongeza BRAC Maendeleo Tanzania kwa kufadhili na kugharamia programu hiyo ya kuendeleza ujuzi iliyolenga kuwajengea walimu na wanafunzi uwezo wa kutumia TEHAMA katika shughuli mbalimbali.

Akizungumza kwa niaba ya shule nufaika, Mkuu wa Shule ya Wailes, Daudi Kassenga, alisema mradi huo umekuwa na manufaa makubwa kwa walimu na wanafunzi kitaaluma kwa kuwa umewasaidia kubuni njia mbalimbali za kufundisha na kuandaa masomo kiurahisi.

"Kabla ya huu mradi, shule zetu za sekondari zilikuwa hazina kompyuta wala maktaba lakini kupitia mradi huu, kila shule imepata kompyuta 20, vishkwambi 20 na kukarabatiwa chumba kimoja cha kuhifadhia vifaa hivyo," alisema.

Naye Anuary Josephat, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Miburani, alisema amefaidika na mradi huo kwa kuwa wakati programu ya mafunzo inaanza alikuwa kidato cha kwanza na ndiyo ilikuwa mara yake ya kwanza kujifunza kompyuta.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa BRAC - Maendeleo Tanzania, Kalunde Simba, alisema utafiti unaonesha changamoto ya wanawake na wasichana wanaojihusisha na masuala ya TEHAMA inachangiwa na ukosefu wa miundombinu ya kutosha na pia ujuzi mdogo wa walimu kuweza kutoa mafunzo husika kwa wanafunzi.

Sambamba na hayo, alisema, pia kumekuwapo na vikwazo vya kijamii na kitamaduni ambapo wazazi wanapendelea wavulana zaidi kulinganisha na wasichana hasa katika elimu, na hiyo imesababisha idadi ndogo ya wasichana kupata mafunzo ya kidigitali, na kupata ujuzi unaohitajika wa kufanya kazi za teknolojia.

Kutokana na changamoto hizo, alisema waliamua kuanza kutoa mafunzo hayo ya TEHAMA shuleni ili wanafunzi wa kike wapate nafasi ya kunufaika na programu mbalimbali zitakazotolewa kipindi cha mafunzo.

Ofisa Elimu Sekondari Wilaya ya Temeke, Niconia Amos, alizipongeza TEA na BRAC Maendeleo Tanzania kwa kutekeleza na kufanikisha mradi wa "Skills for Their Future" katika shule hizo kwa kuwa umekuwa chachu ya maendeleo kwa wanafunzi, hususan wasichana balehe na wanawake vijana.





# TAKUKURU yageukia mifumo ya utendaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani hapa imefanya uchambuzi wa mifumo 11 ya utendaji kazi ili kuboresha huduma katika jamii.

Akitoa taarifa kuhusu uchambuzi wa mifumo hiyo, Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Victor Swella alitaja mifumo hiyo kuwa ni pamoja wa udhibiti wa mapato ya uvuvi katika Wilaya ya Bahi usimamizi wa mawasiliano na utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu Wilaya ya Mpwapwa na wa usimamizi na uendeshaji wa biashara ya nyama wa Wilaya ya Kondoa.

Aliitaja mifumo mingine kuwa ni ushiriki wa wananchi katika miradi ya maendeleo, uagizaji, upokeaji na usambazaji wa vifaa tiba Wilaya ya Kondoa, mianya ya rushwa katika uunganishaji umeme kwa wananchi Wilaya ya Bahi na mfumo msamaha wa matibabu kwa wazee na makundi maalum Jiji la Dodoma.

"Tunafanya hizi chambuzi ili kubaini kama zina changamoto ziweze kufanyiwa marekebisho ili kuondoa usumbufu kwa jamii inayojitokeza kupata huduma kupitia mifumo hiyo," alisema Swella.

Swella alisema taasisi hiyo imeendelea na utoaji elimu kwa jamii kupiga vita rushwa kwa kufikisha ujumbe kwa wananchi kwa mikutano, makongamano na michezo.

Alisema pia wamekuwa wakitoa elimu ya kupiga vita rushwa katika shule za msingi, sekondari, vyuo na kuanzisha klabu za kupinga rushwa.

Swella, alisema klabu hizo zimekuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha jamii kuhusu madhara ya rushwa katika jamii.

# Ni tathmini ya utawala bora, rushwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene amezindua Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa mwaka huu kwa ajili ya kufanya tathmini na utatuzi kero za kisheria kwa wahitaji hasa magerezani.

Akizindua maadhimisho hayo jijini hapa jana, Simbachawene alisema kuwa pia yatatumika kufanya tathmini ya utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa nchini.

"Kwa muda wa miaka miwili mfululizo maadhimisho haya yamefanyika kwa mtindo wa wiki ya huduma kwa umma, wananchi walipata fursa ya kukutana ana kwa ana na watoa huduma na kupata huduma katika Viwanja vya Nyerere Square hapa jijini Dodoma, " alisema.

Alisema kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yatafanyika tofauti kwa watumishi wa umma kufanya kongamano ili kujitathmini kuhusu uzingatiaji wa haki za binadamu na kuepuka rushwa wanapotoa huduma kwa umma.

"Lengo la kongamano hilo ni kuwapa fursa watoa huduma ambao ni watumishi wa Umma kujitathmini ni kwa namna gani wanatekeleza jukumu la Serikali la Ustawi wa Wananchi kwa kuzingatia Haki za Binadamu na kuepuka vitendo vya rushwa na namna wanavyowajibika kwa umma," alisema Simbachawene.

Alisema mada zitakazowasilishwa na kujadiliwa katika kongamano hilo kuwa mbili zinaendana na kauli mbiu 'Haki za Binadamu katika Mapambano Dhidi ya Rushwa" na "Maadili, Haki na Wajibu wa Watumishi wa Umma'.

Waziri huyo, alisema taasisi zinazosimamia utawala bora, zitafanya ziara katika magereza ya Kongwa na Mpwapwa mkoani Dodoma kusikiliza kero na mahitaji ya wafungwa na mahabusu na kutoa misaada ya kijamii.

Alisema kupitia vyombo vya habari viongozi na watumishi wa taasisi watatoa ufafanuzi kuhusu maadili, haki za binadamu na juhudi za vita dhidi ya rushwa nchini.

Alizitaja taasisi zinazoshiriki maadhimisho hayo kuwa ni pamoja na Ofisi ya Rais, Ikulu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Katiba na Sheria, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Tume ya Utumishi wa Umma.

Nyingine ni Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani.



Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, Dk. Maduhu Kazi (kushoto), akikabidhi kompyuta mpakato kwa Ofisa Probesheni wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mwanaidi Makongo, wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Tathmini ya Utekelezaji wa Kazi za Idara ya Huduma za Uangalizi, mjini Singida, mapema wiki hii, ikiwa ni mpango mkakati wa serikali kuhakikisha ufanisi na kasi ya uendeshaji wa mashtaka kwa kutumia mifumo ya kisasa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kupitia mfumo mpya unaojulikana kama 'E-Case Management System', unaotumika nchini kwa lengo la kuharakisha mwenendo wa mashtaka mbalimbali. **PICHA: WMNN**

# Waziri 'amvutia pumzi' mkandarasi

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

NAIBU Waziri wa Maji, Kundo Mathew amekerwa na kitendo cha kusuasua kwa ujenzi wa mradi wa maji katika mji wa Manyoni baada ya serikali kutoa Sh.bilioni 29 kwa ajili ya utekelezaji wake.

Akizungumza juzi baada ya kutembelea mradi huo, Mathew, alisema hajaridhishwa na ujenzi wa tangi la maji litakalohudumia zaidi ya wananchi 64,667 kufikia asilimia 30 kubaki miezi minne kutakiwa kukamilika kulingana na mkataba.

"Sijaridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi huu itabidi pamoja na kwamba sikuwa na mpango wa kuja Januari 2025 Manyoni, itabidi nije tena kukagua kuangalia hatua ulipofikia," alisema.

Alisema atakaporudi mkandarasi aliyekabidhiwa mradi huo ahakikishe amefikia hatua nzuri za ujenzi, vinginevyo, serikali itachukua hatua kali dhidi yake.

Awali, Meneja wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mji wa Manyoni (MAUWASA), Lucas Mwinuka, alimueleza Naibu Waziri kuwa katika mwaka wa fedha wa 2024/2025 mamlaka hiyo itatekeleza miradi mbalimbali kwa ajili ya kuongeza hali ya upatikanaji wa maji katika miji ya Manyoni na Itigi.

Mwinuka, alisema miradi hiyo itagharimu Sh. Milioni 950, kati ya hiyo Sh.milioni 550 wa mji wa Manyoni na Sh. Milioni 400 Itigi na kwamba ipo katika hatua za manunuzi.



## Serikali kuwaunga mkono wadau utalii nchini

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrick Ramadhan Soraga amesema Serikali itaendelea kuwaunga mkono wadau wa maendeleo kwenye sekta ya utalii nchini.

Aliyasema hayo katika mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu kuelekea Tamasha la Tatu la Utalii 'Z- Summit' Zanzibar 2025 visiwani hapa.

Waziri Soraga, alisema tamasha hilo lina mchango mkubwa kwa maendeleo katika sekta hiyo nchini na ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tukio hili ni muhimu katika juhudi zetu zinazoendelea za kuimarisha utalii na maendeleo endelevu Zanzibar," alisema.

Waziri huyo, alisema tamasha hilo litavutia idadi kubwa ya watalii wakiwemo waonyeshaji na wanunuzi kwenye sekta hiyo.

Aliwashukuru waandaaji, wakiwemo jumuiya ya wawekezaji katika sekta ya utalii (ZATI) na KILIFAIR kwa kujitolea kufanikisha jukwaa hilo linalolenga kuitangaza na kuipaisha Zanzibar kupitia utalii.

"Tumejitolea kuimarisha miundombinu, kukuza utofauti na kuvutia uwekezaji ili kufungua uwezo wa sekta yetu ya utalii," alisema.

Aliwataka wafanyabiashara na wadau kutumia jukwaa hilo kufaidika na fursa zilizopo kwenye utalii wa Zanzibar.

Kaimu Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wawekezaji Sekta ya Utalii Zanzibar (ZATI), Suleiman Ali Mohammed, aliishukuru serikali kwa kuunga mkono jitihada za wadau kuinua utalii nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa KILIFAIR, Dominic Shoo, alisema lengo ni kuwakutanisha wadau wakuu wa utalii wakiwemo wawekezaji, mawakala wa usafiri na viongozi wa serikali kwa lengo la kuongeza ajira kwa wananchi na mapato kwa serikali.

Alisema, jukwaa hilo limepangwa kufanyika kuanzia Februari 19 hadi 20,mwakani visiwani hapa.

# Mwinyi kuzindua mazoezi kudhibiti magonjwa yasiyo yakuambukiza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi anatarajia kuzindua siku maalumu ya mazoezi kesho ili kukabiliana na magonjwa yasiyokuwa ya kuambukiza kutokana na takwimu kuonesha kuwa tishio visiwani hapa.

Mpango huo ulitangazwa jana na Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusiana na uzinduzi wa siku hiyo maalum ya kufanya mazoezi kwa wananchi visiwani hapa.

Mazrui, alisema kuwa hatua hiyo imekuja baada ya kuwapo kwa ongezeko kubwa la wagonjwa visiwani hapa.

Aliyataja maradhi hayo kuwa ni kisukari, shinikizo la damu, saratani ya shingo ya kizazi, matiti na tezi dume.

Mazrui, alisema wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wanaendelea na mikakati ili kupunguza ongezeko la magonjwa hayo ambayo yamekuwa yakiigharimu serikali kwa kutumia fedha nyingi za matibabu na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

"Kwa sasa tumeona tuanze kuchukua hatua za haraka kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi ya pamoja katika jamii kwani ni njia ya kupambana na magonjwa haya," alisema.

Alisema kwa sasa vichocheo vya magonjwa hayo ni vingi na kuwa chanzo cha kuongezeka kwa watu wanaokumbwa nayo na kuwa tishio katika jamii.

Alisema utafiti uliofanywa mwaka jana na wizara yake umebaini kuwa ugonjwa wa kisukari umeongezeka kutoka asilimia 3.8 mpaka 7.5.

Vilevile, alisema utafiti huo umeonesha kuwa ugonjwa wa shinikizo la damu umeongezeka kutoka asilimia 33 mpaka asilimia 43.

Alisema uzito na unene wa miili kupitiliza umefikia asilimia 43.4 kutoka asilimia 36.6.

Akizungumzia kuhusu saratani, wanawake 69 waligundulika na ya shingo ya kizazi na kwamba hadi kufikia Machi mwaka huu,wameongezeka hadi kufikia 105 waligundulika na saratani ya shingo ya kizazi, matiti 25.

"Ni vyema kuhamasisha jamii kufanya uchunguzi mapema na kupata elimu kwani maradhi haya yanatibika endapo utagundulika kwa hatua ya awali," alisema Waziri huyo.

Alisema wagonjwa hao wanaendelea kupatiwa matibabu katika hospitali na vituo vya afya vya Unguja na Pemba.




Kamishna wa Polisi Zanzibar, Hamad Khamis Hamad (kulia), akikabidhi zawadi ya mlango wa Zanzibar kama urembo kwa Mkuu wa Polisi Umoja wa Mataifa, Kamishna Faisal Shahkhar alipofika katika makao makuu ya polisi Zanzibar mapema wiki hii. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wizara yafungua kambi magonjwa ya kuhara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imefungua kambi maalumu kwa ajili ya kutoa matibabu kwa wagonjwa wa kuhara eneo la Fuoni Kibondeni Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Waziri wa Wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake baada ya kulipuka kwa ugonjwa huo visiwani hapa.

Mazrui alisema kuwa katika kambi hiyo hadi sasa imepokea wagonjwa 36 wanaoendelea kupatiwa matibabu baada ya kufunguliwa.

Alisema uchunguzi uliofanywa na wizara hiyo umegundua watu waliopatwa na ugonjwa huo wamekunywa maji yasiyo salama kwa afya zao.

Waziri huyo, alisema Hospitali ya Micheweni Pemba imepokea wagonjwa tisa na ya Kivunge 20 na kwamba hakuna aliyefariki.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kujikinga na mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza kwa kuweka mazingira safi, kuosha mikono kwa sabuni na maji tiririka kabla na baada ya kula, kuchemsha maji na kuacha kutupa taka ovyo.

Awali, Mazrui, alisema ugonjwa huo uliibuka hivi karibuni baada ya mvua kunyesha visiwani hapa na kuwataka wananchi wanapoona dalili kuwahi hospitali kupata matibabu ili kudhibiti kusambaa.

Aliwataka wakuu wa mikoa na wilaya kuacha siasa na badala yake kuhamasisha usafi wa mazingira katika maeneo yao ili kudhibiti ugonjwa huo.

"Juzi tu nilitembelea katika Soko la Kinyasini Kaskazini Unguja hali ni mbaya sana, soko chafu halitamaniki," alisema.

Alisema serikali inafanya jitihada ya kujenga masoko ya kisasa hivyo ni vyema kila mmoja kutimiza wajibu kwa kuweka mazingira katika hali ya usafi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



## OMOTOLA AZIDI KUIMARIKA

Uk.14

JUMAMOSI DESEMBA 7, 2024



# 'Wale Wale' kichambo cha gizani

WIKI hii mashabiki wa muziki hawakupewa nafasi ya kupumua, baada ya staa wa Bongo Fleva, Zuchu kuachia nyimbo mfululizo.

Katika msururu wa nyimbo hizo, ngoma inayoitwa Wale Wale, imekuwa gumzo kutokana na aina ya muziki wake na ujumbe unaonekana kama 'kichambo' kwenda kwa watu wasiojulikana.

Wimbo huo ambao Zuchu amemshirikisha bosi na mpenzi wake, Diamond Platnumz, una maneno ambayo yanatafsiriwa kama ujumbe maalum kwenda kwa watu ambao walikuwa kikwazo katika maisha yao.

Licha ya wimbo huo kubeba ujumbe mzito, lakini uwasilishaji wake umekuwa katika mtindo wa kitaarab zaidi, hivyo kuwa na wapenzi wengi wanawake.

Baadhi ya wadau wa muziki walieleza kwamba licha ya wimbo huo kuonekana kupendwa na mashabiki wengi, unaweza kuwa ni moja ya spika lililotumika na wasanii hao kutoa nyongo zao zilizorundikana kwenye mioyo yao kutokana na mapitio yao ya maisha, muziki na hata uhusiano wa kimapenzi.

BASI SAWA

## CassyPool kugombea ugavana

STAA katika mitandao ya kijamii kutoka Kenya, CassyPool, amesema atawania kiti cha ugavana wa Nairobi katika uchaguzi wa 2027.

Amesema katika utafiti wake amegundua katika nafasi hiyo hana ushindani na watu wanaoweza kumkaribia kwa mbali ni gavana wa sasa Johnson Sakaja.

Pia amesema mtu mwingine ambaye anaweza kushindana naye lakini sio kwa ushindi ni mbunge wa Embakasi Mashariki, Babu Owino.



## Wasanii chipukizi waitwa Nafasi Academy 2025

KITUO cha kuendeleza sanaa cha Nafasi Art Space, kimetoa fursa kwa wasanii chipukizi wanaohitaji mafunzo ya fani hiyo kwenda kujiunga.

Uongozi wa kituo hicho ulisema kuwa mafunzo hayo ni fursa ya kipekee kwa wasimamizi na waratibu wa kazi za sanaa kuboresha ujuzi katika kazi zao katika jamii ya fani hiyo.

Uongozi huo ulibainisha kuwa mafunzo yanawapa washiriki fursa ya kuwa sehemu ya juhudi za kuendeleza fani ya sanaa nchini.

Pia kituo hicho ambacho kimeanzishwa kwa ajili ya kupanua wigo wa sanaa nchini, kinatarajiwa kufanya upembuzi wa shughuli mbalimbali kuhusu uendelezaji wa filamu zilizofanywa kwa mwaka huu.

Uongozi wa kituo hicho ulisema kazi hiyo itakuwa ni fursa kwa wajumbe na wadau kusherehekea kazi za wasanii waliofanya vizuri 2024.





# Shamsa anapokumbuka filamu ya Chausiku

MWIGIZAJI mkongwe Shamsa Ford, ameikumbuka filamu ya Chausiku, akisema katika maisha yake ya sanaa ndiyo ilimpatia kipato kikubwa.

Shamsa ambaye amekuwa akitoa picha mbalimbali za zamani kama kumbukumbu zake, amesema baada ya kutoka filamu hiyo alitengeneza fulana zilizoandikwa 'Nampenda Chausiku' ambazo aliziuza na kumpatia kipato kikubwa.

"Baada ya filamu ya Chausiku kufanya vizuri, basi nikajiongeza nikatengeneza fulana, niliuza mno na kujipatia riziki kubwa .Alhamdulillah ukifanya kazi nzuri watanzania wanaona na kukuunga mkono," amesema Shamsa.




# Vichwa maji: Pembe na Senga

**Na Adam Fungamwango**

OKTOBA 20 mwaka huu, tasnia ya sanaa nchini Tanzania ilipata pigo zito kwa kuondokewa na msanii mkongwe nchini, Yusuph Kaimu, maarufu kwa jina la Pembe.

Msanii huyo mwigizaji wa filamu za vichekesho, alifariki dunia kwenye hospitali ya Temeke alipokuwa akipatiwa matibabu.

Pembe alianza kuigiza tangu miaka ya 1980 alipokuwa akifanya maonesho ya majukwaani akiwa na makundi mbalimbali vya sanaa za utamaduni, ikiweno DDC Kibisa Ngoma Troupe.

Mageuzi ya kuingia kwa televisheni nchini, hayakumpita Pembe, kwani aliamua kuingia kuigiza kwa njia hiyo na kuzidi kujipatia umaarufu mkubwa.

Alizikwa Oktoba 21 mwaka huu kwenye makaburi ya Msikiti Mweupe, eneo la Yombo Dovya Jijini Dar es Salaam.

Leo tunamuenzi kwa filamu yake moja ambayo alicheza na 'pacha' wake Senga. Mara nyingi filamu wanazocheza pamoja siku zote zinakuwa na mvuto mkubwa. Inaitwa 'Vichwa Maji'.

Mbali na wasanii hao, imechezwa pia na wasanii Zimwi na Fetty. Ni filamu inayoonyesha kuwa mapenzi ni kitu ambacho hakipimiki.

Senga anapita kwa jirani yake Pembe. Anamuona mke wa jirani yake anaingia bafuni. Kama kawaida ya vyoo na mabafu ya uswahilini yalivyo. Senga anaamua kwenda mlangoni kumchungulia.

Wakati anafanya hivyo, Pembe alimuona. Alimnyatia wakati Senga akili yake iko kwa anachokiona ndani ya bafu.

Anamkamata. Akampa kipigo kizito kiasi cha mke wa Pembe pamoja na kufanyiwa udhalilishaji, akamtaka mumewe aache kumuadhibu mwanaume mwenzake. Hiyo ikaamuudhi Pembe na kumwambia huenda wako kwenye njama moja. Ugomvi ukahamia kwa mkewe. Lakini baadaye wakayamaliza kama mtu na mkewe.

Zimwi yeye ni mume bwege. Anampelekea mkewe maji ya kuoga bafuni. Mkewe anaondoka kwenda kwenye starehe, yeye anafua, kuosha vyombo na kupika. Mkewe akirudi anadai msosi.

Siku moja akarudi na bwana kabisa nyumbani. Fetty ambaye ni mke wa Zimwi alirudi na bwana nyumbani. Hilo lilimkera sana Zimwi. Akachonga sana. Lakini mke akampetipeti, yakaisha.





# Barnaba kawa mwamba

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Barnaba amesema katika miaka 20 ya mafanikio katika muziki hahitaji kiki za kumpandisha chati.

Akizungumza hivi karibuni, amesema kwa bahati mbaya kutokana na kuwa katika uhusiano imara wa ndoa, kila yanapotokea matatizo watu wanachukulia kama anafanya njia ya kusukuma ngoma zake.

"Ndoa yangu iko imara, lakini kuna kipindi kunaweza kutokea kutokubaliana kwa bahati mbaya hapo watu wanaunga matukio kama nataka kusukuma kazi yangu. Ukweli sihitaji nguvu ya ziada kutangaza nyimbo zangu," amesema Barnaba.

# Masongi matano ya kihindi yaliyotisha

**Na Adam Fungamwango**

KWA wale vijana au watoto katikati ya miaka ya 1980 hadi katikati ya miaka ya 1990, wanakumbuka jinsi kulivyokuwa na filamu nyingi kali za kihindi.

Achilia mbali kile kizazi cha mwanzoni mwa miaka ya 1980, kilichokuwa kikienda Drive Inn Cinema, Odeon, Avalon, ambapo mitaani hakukuwa na video wala televisheni, kulikuja kizazi kingine ambacho tayari video angalau moja moja zilianza kuonekana mitaani.

Badala ya watoto kwenda kwenye majumba ya sinema na ilikuwa kwao ni ngumu kidogo, sasa walianza kwenda kwenye nyumba za watu ambao walikuwa wakionyesha filamu mbalimbali. Kila mkoa nchini Tanzania kulikuwa na sehemu ambazo watoto walikuwa wakienda filamu.

Dar es Salaam, hasa maeneo ya Kinondoni kulikuwa na sehemu maarufu kama 'Milano' na 'Morocco', karibu kabisa na Kanisa Katoliki Magomeni.

Kwenye filamu za Kihindi, mbali na utamu wa filamu zenyewe, lakini vijana na watoto walipenda sana nyimbo zake.

Hapa leo tutaangalia baadhi ya masongi ya Kihindi yaliyotamba na kupendwa sana enzi hizo.

**Goron Ki na Kalon Ki**

Ni moja kati ya 'songi' maarufu sana kwa vijana na watoto wa miaka ile ya 1980 hadi 1990. Sidhani kama kuna aliyekuwa mtoto au kijana licha ya kwamba sasa atakuwa mtu mzima, asiufahamu.

'Goron Ki na Kalon Ki' ni wimbo ambao upo kwenye filamu ya 'Disco Dancer' ambayo staa wa picha alikuwa ni Mithun Chakraborty.

Filamu hii maarufu sana na iliyotokea kupendwa ilitoka mwaka 1882, na ilikuwa na 'masongi' mengi makali 'Goron Ki na Kalon Ki, Duniya Hai Dilwalon Ki.' Hiyo ni sehemu ya wimbo huo.

**Jimmy Jimmy aaja**

Hapa sasa ndiyo balaa. Hili 'songi' la Jimmy, ukikuta watoto mtaani wanaliimba utafurahi na roho yako.

Halafu kila mmoja anaujua wimbo huu kikamilifu kwa sababu ni sehemua ambapo staa wa picha Mithun anakwenda kushika gitaa lililotegwa umeme, mama yake atakuja kumuokoa. Filamu ni hiyo hiyo Disco Dancer.

**Juma Chuma Dede**

Mwaka 1991 kulitoka filamu moja kati kali ya Kihindi iliitwayo 'Hum'. 'Starlingi' wake ni Amitabh Bachchan.

'Juma Chuma Dede' ni moja kati ya 'songi' lililopendwa sana na mashabiki wengi wa picha za kidosi au filamu za Kihindi wakati huo. Na hata hapa nchini bendi ya Varda Arts imesahawahi kuchukua mirindimo ya wimbo huo na kuimba kwa kiswahili.

**Kuch Kuch Hota Hai**

'Songi' hili kali lipo kwenye kwenye filamu kali ambayo inaenda kwa jina hilo hilo. Ilitoka mwaka 1998 na kuushtua ulimwengu wa filamu za Kihindi duniani. Staa wa picha hiyo ni Shah Rukh Khan, huku wimbo huo ikitia fora na kupendwa na watu wengi zaidi kuliko wimbo wowote ule kwenye picha hilo.

**My Tarzan**

Tarzan ni moja kati ya filamu maarufu mno nchini Tanzania na duniani kote. Ilikuwa ni filamu iliyoonyesha kuwa mapenzi yanaweza kumea popote pale hata pasipo na mbolea, porini na kwa mtu yoyotre yule. Ndani yake kuna 'masongi' kibao mazuri, lakini uliokuwa rahisi zaidi kuimbwa na Wabongo uliitwa 'My Tarzan', ambao ulifunika bovu.






# Timaya hataki ndoa

MWANAMUZIKI wa Nigeria Timaya amesema hajafikiria kuingia katika maisha ya ndoa kwa sababu anaamini itakuwa vigumu kwake.

Wakati wa mahojiano yake ya hivi karibuni, Timaya amesema tangu awe mvulana mwenye sifa ya kuoa, yeye ndiye alikuwa akiwaacha wanawake waliokuwa kwenye uhusiano wa kimapenzi kwa kuwa hataki kuwa na msongo wa mawazo.

"Naangalia kama nitaoa leo nitaweza kutoka? mahusiano yangu yote ya awali, mimi ndiye niliyetoka kwa sababu sipendi msongo. Nitabaki katika maisha haya kwa muda mrefu," amesema.



## Funke Akindele atambulisha filamu mpya

MSANII wa filamu kutoka Nigeria, Funke Akindele, amewapa msisimko mashabiki zake katika filamu yake mpya inayoitwa Everybody Loves Jenifa, iliyopangwa kutoka mwezi huu.

Katika filamu hiyo ambayo imewashirikisha wakongwe kama Toyin Abraham na King Sunny Ade ambayo inaonekana kuwa ya moto zaidi.

Funke Akindele katika mradi wake huo amewaingiza wanamuziki wakongwe Lagbaja na D'banj katika kunogesha zaidi.

## Moto wateketeza nyumba ya Mercy Aigbe

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Mercy Aigbe, amefichua kuwa nyumba yake ya gharama kubwa iliyoko jijini Lagos iliteketea kwa moto.

Mercy ametumia ukurasa wake wa Instagram kuchapisha video inayoonyesha uharibifu uliosababishwa na moto katika nyumba hiyo ya kifahari.

Baadhi ya vitu vilivyoonekana vimeteketea ni mapazia, sofa na vitu mbalimbali vilivyokuwemo ndani ya nyumba hiyo.





## Davido eti nini?

MWIMBAJI maarufu wa Nigeria, Davido, amefunguka akisema haoni tatizo uvutaji wa bangi, licha kuwa katika kundi la dawa za kulevya.

Akizungumza hivi karibuni, Davido amesema anatoa mchango katika kupambana na matumizi ya dawa za kulevya na kusaidia vituo vya watoto yatima katika siku yake ya kuzaliwa kama shukrani zake.


Amesisitiza dhamira yake ya kukabiliana na matumizi ya dawa za kulevya kupitia juhudi zake za uhisani, lakini anachoamini matumizi ya bangi hayana adhari kubwa kuliko dawa zingine.

## Omotola azidi kuimarika

MWIGIZAJI wa Nollywood, Omotola Jalade Ekeinde, amesema afya yake inazidi kuimarika baada ya kufanyiwa upasuaji wa kuondoa kifuko cha nyongo ambacho kilikuwa kikimsababishia maumivu.

Staa huyo wa filamu alitumia ukurasa wake wa Instagram kutoa shukrani zake kwa mafanikio ya upasuaji huo na kuelezea jinsi alivyopambana na hali ngumu.

Mama huyo wa watoto wanne, akiwa hospitalini amesema ugonjwa huo ulikuwa mgumu sana kiasi cha madaktari kuchukua hatua ya dharula ya kumfanyia upasuaji.





# Tanzania yavunja rekodi kwa uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Gilead Teri amesema Tanzania ipo kwenye nafasi ya kuvunja rekodi ya miaka 11 ya usajili wa miradi mingi ya uwekezaji.

Hadi kufikia Novemba 29, mwaka huu, TIC ilikuwa imesajili miradi 800, idadi ambayo iko karibu kufikia rekodi ya miradi 865 iliyosajiliwa mwaka 2013.

Teri aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati akizungumza na wadau na wafanyabiashara katika hafla ya kumbukizi ya miaka 20 tangu kuanzishwa Kampuni ya Vinywaji ya Mega Beverages.

"Mwaka huu tunaweza kuvunja rekodi. Tangu kuanza rasmi usajili wa miradi mwaka 1997, mwaka 2013 ndio unaoshikilia rekodi, lakini sasa tuna nafasi nzuri ya kuvuka idadi hiyo kutokana na ongezeko la miradi," alisema.

Alisema kati ya miradi iliyosajiliwa, 260 ni ya wazawa ya sekta ya ujenzi, kilimo, uchukuzi, utalii, na majengo.

Kuhusu mazingira bora ya Uwekezaji, Teri, alisema ni matokeo ya mageuzi makubwa katika kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini.

Alibainisha kuwa kwa sasa Tanzania ina sera thabiti, rasilimali nyingi, nishati ya uhakika, soko kubwa na nguvu kazi inayokidhi mahitaji ya wawekezaji.

"Tanzania imekuwa mahali pazuri kwa wawekezaji. Mazingira ya sera ni rafiki na rasilimali zilizopo zinatoa fursa kubwa kwa uzalishaji wenye tija," alisema.

Akizungumza kuhusu mafanikio ya Mega Beverages, Teri, alisema kufikisha miaka 20 ni ushahidi wa uwezo wa wazawa katika sekta yenye ushindani mkali.

"Sekta ya vinywaji nchini ilifikia thamani ya Dola za Marekani bilioni 3 (Sh trilioni 8) mwaka 2023, huku vinywaji vikali vikichangia Dola milioni 721 (Sh trilioni 1.8) asilimia 80 hadi 90 ya vinywaji vilivyouzwa mwaka huo vilizalishwa nchini, hususan bia," alisema.

Teri alisema lengo ni kupunguza zaidi bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ndani ya miaka miwili ijayo wakati ambao TIC inavutia wawekezaji wa kimataifa kuhamishia uzalishaji wao nchini.



Mkuu wa Wilaya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lazaro Twange (kushoto), akikabidhi bendera ya taifa kwa Kanali Deus Babuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), katika lango Marangu juzi, ili kuipandisha katika kilele cha Mlima Kilimanjaro, kwa ajili ya kuadhimisha miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika Desemba 9 mwaka huu, akiongoza kikosi cha wananchi 300.
**PICHA: MARY MOSHA**

# Mnyororo waboresha maisha ya wakulima

**Na Allan Isack,** ARUSHA

ZAIDI ya wakulima 73,000 nchini wamenufaika na mradi wa mnyororo wa thamani unaostahimili hali ya hewa kwa ajili ya kuboresha maisha (CRAFT).

Hayo yalisemwa jana na Katibu Tawala Msaidizi Huduma za Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Arusha, Daniel Oruku wakati akifungua mkutano wa tathimini ya changamoto na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wadau wa kilimo.

Oruku, alisema mradi huo unaotekelezwa na shirika lisilokuwa la kiserikali la SNV umewafikia wakulima zaidi ya 73,000 kupitia kwa vyama vya ushirika na watoa huduma sawa na asilimia 71 ya wakulima wadogo mmoja mmoja.

Alisema kati ya wakulima hao, 29534 sawa na asilimia 40 wameongeza uzalishaji wa mazao na kuongeza kipato kwa kutumia teknolojia na mbinu himilivu zinazoelekezwa na maofisa ugani na wakulima viongozi kwenye mashamba darasa.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje ya Uholanzi, umekuwa ukiwashirikisha wadau wa kilimo tangu mwaka 2018. Vilevile, Oruku, alisema mradi huo umevishirikisha vyama vya ushirikia 21 wakihamasisha kilimo kwa mazao ya viazi mviringo, maharage, mtama na alizeti.

"Mkutano huu utajikita zaidi katika kilimo cha maharage kwa kuwa zao hilo linagusa makundi ya vijana na wanawake, linapatikana kwa urahisi na kustahimili ukame na linastawi sehemu nyingi nchini," alisema.

Alisema tangu mwaka 2018, Mradi wa CRAFT ulipozinduliwa nchini umekuwa na matokeo chanya kwa wanufaika kwa kuwa wameweza kulima kilimo chenye tija na kuongeza kipato.

"Kutokana na ongezeko la shughuli za kibinadamu kumekuwa na ongezeko la athari za mabadiliko ya tabia nchi kwa kuwa imeathiri shughuli zote za kilimo hivyo sio jambo la kufumbia macho kunahitajika njia mbadala za kukabiliana nalo,"alisema.

Godfrey Kabuka,Ofisa Mshauri Mwandamizi wa Kilimo wa CRAFT kutoka SNV, alisema wameandaa mafunzo ya mabadiliko ya tabianchi kwa wadau wa zao la maharage kwa lengo la kuwajengea uwezo. Kabuka, alisema zao hilo nchini limekuwa likilimwa zaidi na wanawake na vijana na kustawi kwenye mikoa mbalimbali nchini.

Alisema wamefikisha mbinu za kilimo himilifu kwa wakulima wengi na kufanikiwa kuongeza uzalishaji wa zao hilo.

"Changamoto kubwa inayoikumba zao la maharage ni ukame, mvua kunyesha kupita kiasi na wadudu wengi hasa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini," alisema Kabuka.

Dk.Mathusela Michael wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dawati la Uratibu wa Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali, alisema mradi huo umewanufaisha wakulima wengi hasa wadogo wa vijijini.

# Shamrashamra za Uhuru zapamba moto

**Na Mary Mosha,** MOSHI

JENERALI Mstaafu wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), George Waitara amekabidhi rasmi bendera kwa Kanali Deus Babu kwa lengo la kuipandisha na kuisimika kilele cha Mlima Kilimanjaro ikiwa ni Maadhimisho ya Miaka 63 ya Uhuru wa Tanganyika yanayotarajia kufanyika nchini kesho kutwa.

Tukio hilo lilitokea kwenye lango kuu la Marangu chini ya uratibu Kampuni ya Zara Advantures.

Waitara, alisema ni wakati mwafaka kwa watu kujitokeza kusimamia rasilimali za taifa na kuzitangaza ili kukuza mapato ya nchi.

"Idadi ya wapandaji inaongezeka siku hadi siku, Mwaka 2018 tulipanda watu takribani 10, mwaka 2024 takribani 300, 237 wanapandishwa, hii inaonyesha kuwa watu wanahamasika kupanda mlima huu," alisema na kuongeza kuwa:

"Nitoe wito kwa wapandaji wote kufuata ushauri wa waongozaji hasa katika jambo la Pole Pole, 'Usipouheshimu mlima na wenyewe unakudharau na huwezi kufika kileleni."

Mgeni rasmi, Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lazaro Twange kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema serikali mkoa huo umejipanga kutatua matatizo yanayojitokeza ili kupunguza maswali kwa wawekezaji.

"Mabalozi huko mlipo hakikisheni mnajitangaza vyema ili kuleta watalii wengi zaidi na sisi huku tutafanya kila linalowezekana kuweka mazingira ya uwekezaji vizuri na kuzungatia ushauri ili kuboresha zaidi," alisema.

Ofisa Tawala na Utumishi wa kampuni hiyo, Benard Saini, alisema wamepandisha Watanzania katika makundi 237 katika mlima huo kwa mwaka huu.

Saini, alisema wamejipanga na timu ya uokoaji kwa kutumia ndege za dharura ili kuhakikisha atakayepata matatizo njiani anarejea akiwa salama.

"Waliopanda ni 237 kupitia lango la Marangu, ila ni watu takribani 600 wameingia mlimani hii leo,"alisema.

Akipokea bendera hiyo, Kanali Babuu, alisema kundi hilo la watu takribani 300, baadhi wamepanda kwa lango la Marangu na Lemosho na Machame na kwamba wanatarajia kufikisha bendera hiyo Desemba 9, mwaka huu katika kilele hicho.

Amidi wa Mabalozi, Maadhi Maalum , alisema kupanda mlima huo hujenga uraibu na mtu uzalendo wa kuendelea kuupanda mara kwa mara.

"Leo tunapanda mabalozi tisa wanaowakilisha Tanzania nchi mbalimbali duniani, wengine kumalizia viporo walivyoacha mwaka jana, kutangaza mlima wetu na wengine kujionea ili kujifunza zaidi na kwenda kuhamasisha wageni katika nchi walizopo," alisema Maalum.

## TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Nzaya Nzayadio, uliowachezesha watu Cavasha, endelea kupumzika kwa amani

**Na Adam Fungamwango**

LEO ni miaka minne kamili tangu alipofariki mwanamuziki nyota kabisa wa nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kuanzia miaka ya 1970 hadi mwishoni mwaka miaka ya 1980, Nzaya Nzayadio.

Mwanamuziki huyo alifariki dunia Hull City nchini Uingereza Desemba 7 mwaka 2020 kwa ugonjwa wa COVID-19, unaosababishwa na virusi vya corona, akiwa na miaka 65.

Kwa vijana wa sasa wanaweza kushangaa na kuanza kujiuliza mara mbili mbili ni nani, lakini wale waliokuwa vijana au watoto miaka hiyo niliyoitaja hapo juu, sijui kama hawazifahamu nyimbo zilizokuwa zikitamba wakati huo zikiimba kwenye mabaa, magari, hoteli na hata vituo vya usafiri kama 'Kendeke Malembe eee eee na lavi Malembe, ngai mama nakoloba.' Hayo ni baadhi ya maneno ambayo yamo kwenye wimbo wa 'Kendeke Melembe'. Ni moja kati ya kazi nzuri na mwanamuziki huyo. Wale watoto wa Dar es Salaam miaka hiyo au waliowahi kuishi wakati huo ambao kwa sasa ni watu wazima na wametapakaa nchini hata nje ya nchi watakumbuka kulikuwa na gari moja linafanana na Hiace hivi, lilikuwa likizunguka jiji zima likiuza 'Ice Cream' aina ya koni na hata zile za kwenye vikopo vidogo vya pastiki, nyimbo za Cavasha ambazo nyingi zilikuwa ni za Les Kamale, Orchestra Kiam na Orchestra Lipua Lipua zilikuwa zikitawala kwenye gari hilo.

Watoto wakisikia nyimbo hizo tu, basi wanaanza kuomba pesa kwa wazazi wao au kulia, ili wanunuliwe koni.

Sauti ya Nzaya Nzayadio ndiyo ilikuwa ikisikika zaidi kwenye nyimbo nyingi, akiwa na Orchestra Lipua Lipua.

Ni mwanamuziki raia wa Kongo aliyezaliwa mwaka 1955, lakini mashabiki wa muziki wa Tanzania wa wakati huo hasa wa Cavasha walimtambua kutokana na nyimbo zao nyingi kutamba nchini hata kwenye harusi, kumaliza shule, sikuukuu mbalimbali na hafla za chama na kiserikali.

"Oo tango mosusu ndoki yeye, ooo tangu masusu ndoki Maluku, tango mosusu soki Nzaya, ndoki Nzaya, tango mosusu ndoki tonelo, ndoki Tonelo, ndoki Tonelo, tango mosusu ndoki bino, ndoki bino." Ni baadhi







Santuri za nyimbo matata, Matoba na Ndukidi ambazo zote zilitungwa na mwanamuziki huyo na kuchengua sana mashabiki wa muziki Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.



Mwanamuziki Nzaya Nzayadio

ya maneno maarufu sana kwa Wabongo kwenye wimbo wa 'Ndukidi' ambao Wabongo nao walikuwa wakiweka maneno yao ya kiswahili wanayojua wenyewe, ili mradi tu na wao wafurahi. Hiyo ilikuwa ni sauti nzito ya Nzaya Nzayadio ambaye alikuwa akiitikiwa na mwimbaji mwenye sauti ya kwanza kali, Kilola Tokodiangani ambaye yeye bado yupo hai.

Lakini pia Wabongo wanamkumbuka kwa wimbo wa 'Sekizengi' ambao unapoanza tu, anaanza kwa kusema 'Nzaya Nzayadio na Sekizengi'.

Ukiachilia mbali nyimbo hizo, mwanamuziki huyo akiwa na bendi ya Lipua Lipua, ametunga au kuimba nyimbo nyingi akizotunga mwenzake zilizolipatia umaarufu sana kundi hilo na kuwa tishio.

Mbali na Kilola Tokodiangani, lakini pia alishirikiana na wanamuziki kama Lusuama Aspro na Mongoley Santana kwenye gitaa la solo na mchawi wa gitaa la rhythm na mtunzi wa nyimbo nyingi maarufu za bendi hiyo, Vata Mombasa 'Jujuman', Maluku na wengineo.

Nyimbo zingine zilizotamba sana akiziimba marehemu kwa umahiri mkubwa ni 'Mfueni', 'Matoba', 'Mbondo', 'Naleli Libala', 'Lemba Lemba','Temperature, 'Nouvelle Generation' na nyingine nyingi.

Mwanamuziki huyo, kabla ya kufariki alilazwa kwa wiki mbili kwenye Hospitali ya Hull Royal Infirmary mjini Hull City nchini Uingereza, akiugua ugonjwa huo ambao mpaka sasa bado ni janga la dunia.

Ana historia kubwa kwenye ulimwengu wa muziki, lakini umaarufu wake ulianza mwaka 1973 alipojiunga na Orchestra Lipua Lipua kwenda kuziba pengo la sauti nzito ya Pepe Kalle aliyekuwa amejiengua na bendi hiyo kwenda kuunda bendi yake ya Empire Bakuba, akiwa na Papy Tex na Dilu Dilumona, pia Nyboma mwenye sauti ya kwanza aliondoka na kuchukuliwa Kilola Tokodiangani kuziba pengo pia na kuanza kuuwasha moto.

Ni mmoja wa wanamuziki walioleta mapinduzi makubwa ya muziki kutoka ule wa rhumba wa kina Franco na Tabu Ley na kuleta wa vijana ambao ulikuwa na mapigo ya kasi wao wakaita 'Cavasha'.

Hadi anafariki mwanamuziki huyo alikuwa akiishi nchini Uingereza, akiendelea na mambo ya muziki, lakini alikuja nchini Tanzania miaka michache tu iliyopita akiwa mwenyeji wa mwanamuziki mwenzake Tshimanga Kalala Assosa ambaye walikuwa wote kwenye bendi ya Lipua Lipua, kabla ya kina Assosa na Nyboma kwenda kuunda bendi ya Les Kamale.

Ni mwimbaji mwenye sauti nzito, ambayo ukiisikiliza inashabihiana na ya Pepe Kalle au Madilu System.

Kutokana na kuishi nchini Uingereza, ambako kuna teknolojia kubwa zaidi, alikuwa ameshaanza kuziondoa nyimbo zake nyingi na bendi yake ya Lipua Lipua kwa mtindo wa Audio na kuziweka kwa mtindo wa video.

HABARI KIMATAIFA

# MSAKO KOREA KUSINI

## -Wakuu wa ujasusi wasimamishwa

VYAMA vikuu vya kisiasa vya Korea Kusini vinafanya mazungumzo ya dharura, wakati wabunge wakiendelea kujadili kuharakisha upigaji kura ya kumtimua madarakani Rais Yoon Suk Yeol.

Hata hivyo, kiongozi wa chama tawala cha PPP, Han Dong-hun, katika mkutano wa chama hicho alisisitiza haja ya kusimamisha haraka majukumu ya rais Yoon.

Dong-Hun alisema rais alichukua hatua ya kutisha na vitendo vya hatari kutokana na tamko lake la kuiweka nchi hiyo chini ya amri ya kijeshi.

Kiongozi huyo wa wabunge wa chama tawala alisema anazo taarifa kwamba rais aliamuru hata kukamatwa kwa viongozi wa kisiasa.

"Nilisikia kutoka kwa chanzo cha kuaminika kwamba Rais Yoon Suk Yeol aliamuru utawala wa amri ya kijeshi utakapoanza kamanda wa ujasusi awakamate viongozi wakuu wa kisiasa, kwa tuhuma za kula njama dhidi ya serikali," alisema.

Aliongeza "Rais alikataa kukubali kwamba haikuwa njia sahihi kutangaza sheria ya kijeshi."

Kiongozi huyo wa chama alisema ikiwa Rais Yoon Suk Yeol ataruhusiwa kuendelea na shughuli za serikali, kuna hatari ya kufanya matendo makubwa zaidi kama vile kujaribu tena kuweka sheria ya kijeshi, jambo ambalo linaweza kuiweka Jamhuri ya Korea na raia wake katika hatari kubwa.

Wizara ya Ulinzi ya Korea Kusini, ilitoa tangazo la kumsimamisha kazi kamanda wa idara ya ujasusi, Yen In-Hyung, ambaye imedaiwa alipewa amri ya kuwaweka kizuizini wanasiasa.

Taarifa ya wizara hiyo iliendelea kusema kwamba maofisa wakuu wengine wawili, akiwemo kamanda wa kamandi maalumu wa vita, wamesimamishwa pia kazi.

Pia mwendesha mashtaka wa Korea Kusini ametoa amri ya kutosafiri nje ya nchi kwa maofisa kadhaa wa jeshi.

Wanasiasa waliolengwa kukamatwa kufuatia amri ya rais ni pamoja na kiongozi wa chama tawala bungeni, kiongozi wa upinzani na Spika wa Bunge la Kitaifa.

Lakini Mkurugenzi wa shirika la kijasusi alitilia shaka taarifa hizo, akieleza kwamba hakuwahi kupokea maagizo yoyote kutoka kwa rais ya kuwatia mbaroni wanasiasa hao.

Wakati hali inazidi kuwa mbaya kwa Rais Yoon Suk, wafuasi wa upinzani walikusanyika kwenye majengo ya bunge wakiwa na mabango wakitaka rais aondolewe madarakani.

Vyama vya upinzani vinashinikiza leo kuanza mchakato wa kupiga kura ya kutokuwa na imani na rais Yoon, wakiita amri yake ya sheria ya kijeshi ya muda mfupi kuwa ni tamko lililo kinyume cha katiba na uasi au mapinduzi.

Hata hivyo, upinzani una viti 192 katika Bunge la Kitaifa lenye wabunge 300, wanahitaji kuungwa mkono na wabunge wa chama tawala.

Jaribio la Rais Yoon kuanzisha sheria ya kijeshi lilishtua nchi, marafiki wa Korea Kusini na masoko ya fedha. Alilitengua muda mfupi baada ya wabunge wa nchi hiyo kupitisha haraka sheria ya kuzuia tangazo hilo.

**DW**



Waasi wa Syria wakiwa kwenye viunga vya mji wa Homs jana baada ya wanajeshi wa serikali kuondoka. **PICHA: AP**

# Waasi Syria wazidi kuelekea Damascus

**DAMASCUS,** SYRIA

RAIS wa Syria, Bashar al-Assad ameapa kuwaponda waasi ambao amewataja kama magaidi katika mapigano mapya yaliyozuka hivi karibuni.

Akizungumza kwa njia ya simu na Rais wa Iran, Masoud Pezeshkian, Assad aliilaumu Marekani na nchi nyingine za Magharibi kwa mashambulizi hayo, akisema wanajaribu kuchora upya ramani ya eneo hilo.

Pezeshkian alisisitizia Iran inasimama imara pamoja na serikali ya Syria na watu wake na kuongeza kuwa kuhifadhi mamlaka ya Syria na uadilifu wa ardhi yake ndio msingi wa mkakati wake wa kikanda.

Wakati huo huo msemaji wa Ikulu ya Russia, Dmitry Peskov, alisema nchi yake inafuatilia kwa makini hali ya mambo inayoendelea karibu na jiji la Aleppo na inachukulia mashambulizi ya waasi kama shambulio dhidi ya uhuru wa Syria.

Peskov alisema Russia ingependa kuona mamlaka ya Syria ikileta utulivu katika eneo hilo na kurejesha utaratibu wa kikatiba haraka iwezekanavyo.

Wakati huo huo, maelfu ya watu wanaukimbia mji wa tatu kwa ukubwa nchini Syria wa Homs kwa hofu ya waasi wanaoongozwa na Waislamu wataendelea kusonga mbele kuelekea mji mkuu, Damascus.

Waasi waliuteka mji wa Homs ulioko kaskazini juzi likiwa pigo la pili kubwa kwa Rais Bashar al Assad ambaye alipoteza udhibiti wa Aleppo wiki iliyopita.

Kiongozi wa kundi la wanamgambo wa Kiislamu la Hayat Tahrir al-Sham (HTS), walifanya mashambulizi ya kushtukiza dhidi ya serikali na hadi sasa wameteka miji miwili mikubwa.

Homs ni mji unaofuata kwenye barabara ya kutoka Aleppo kuelekea Damascus.

Watu waliokuwa na hofu kutoka jamii ya Alawi anayotoka Rais Assad wanaondoka katika mji wa Homs, wakiwa na video zinazoonyesha barabara zilizojaa magari.

**BBC**

# DRC yafuatilia kwa karibu mlipuko ugonjwa mpya

**KINSHASA,** DRC

SERIKALI ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imetangaza kuwa iko katika tahadhari ya juu kutokana na mlipuko wa ugonjwa usiojulikana ambao umesababisha vifo vya watu kadhaa ndani ya mwezi mmoja.

Waziri wa Afya, Samuel Roger aliwaambia waandishi wa habari juzi mjini Kinshasa kuwa mamlaka iko macho na kwamba wanafuatilia mlipuko wa ugonjwa huo kwa ukaribu.

Waziri huyo alisema kuwa wamehesabu miili ya watu 27 katika vituo vya afya waliokufa kutokana na ugonjwa huo.

Ugonjwa huo unasababisha dalili zinazofanana na mafua makali ambazo ni homa, kikohozi na maumivu ya kichwa.

Ugonjwa huo uligunduliwa kwa mara ya kwanza mwishoni mwa mwezi Oktoba na hadi sasa umeripotiwa zaidi katika eneo la Panzi, takriban kilomita 700 kusini mashariki mwa mji mkuu Kinshasa.

Aliongeza kuwa watu wengine 44 wameripotiwa kufariki lakini huenda vifo hivyo vimetokana na sababu nyingine.

**DW**

# Wazabuni, makandarasi wazawa wajadili njia kufikia miradi WB

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imewakutanisha makandarasi na wazabuni wa ndani wanaohitaji kufanya kazi katika miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia (WB) ili kuwajengea uwezo na kusikiliza changamoto zinazowakabili.

Mkutano huo uliofanyika juzi jijini Dar es Salaam, uliandaliwa na WB na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) Bara na Visiwani Zanzibar.

Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha, Elijah Mwandumbya, akizungumza wakati akifungua mkutano huo, alisema serikali itaendelea kuwajengea uwezo wadau hao ili kushiriki kikamilifu zabuni zinazotoka nje ya nchi.

Alisema wakijengewa uwezo watapata kipato, kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, ujuzi na kuongeza mitaji yao katika kazi zinazotolewa na serikali.

Alisema katika kutimiza mikakati hiyo mwaka 2023, serikali ilipata kibali cha Bunge, kufanya maboresho na kuanzisha sheria mpya ya ununuzi wa umma ambayo imetoa fursa zaidi kwa Watanzania.

"Sheria hii ipo kwa ajili ya kutafsiri maono ya Rais Samia Suluhu Hassan, lakini katika kazi ambazo zitazidi kiwango hicho, kampuni za Tanzania zinauwezo wa kuzifanya kwa ushirikiano na kampuni za nje," alifafanua Meandumbya.

Alisema pia, wametafsiri namna wanavyoweka upendeleo kwa Watanzania hasa maeneo yanayotumia rasilimali au malighafi za ndani ya nchi na yale yanayoajiri wazawa.

Kamishna anayesimamia Maendeleo ya Sera za Ununuzi wa Umma na Ugavi wa Wizara ya Fedha, Fredrick Mwakibinga, alisema mkutano huo umegusa namna ya kupata fursa ya kupata miradi hiyo.

Alisema pia, changamoto wanazokabiliana nazo makandarasi pamoja na kuona namna ya zabuni zinavyogawanyishwa kwa makandarasi wazawa na wa nje.

"Katika ununuzi wa umma umegawanyisha zabuni kwa upendeleo maalum kwamba, kunapokuwa na zabuni ya Sh. milioni 50, inabidi iende kwa kampuni za kitanzania.

"Hii imefanywa na serikali kutokana na kuzuia watu wa nje kutokuja kuwanyang'anya watu wa ndani tenda na huu ni upendeleo rasmi umeona uzuie baadhi ya maeneo ili Watanzania washiriki," alisema.

Naye Meneja Uendeshaji wa WB nchini, Milena Stefanova, alisema miradi yao ina masharti kwa sababu wanataka ijengwe kwa kuzingatia sifa na vigezo.

Alisema wamekaa pamoja na kukumbushana mambo muhimu ya kuzingatia ili wanufaike na fursa zinazotolewa na benki hiyo.




Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge (katikati), akiwa pamoja na madaktari 20 katika Uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kuwasili wakitokea nchini Comoro, walikoweka kambi maalum ya matibabu ya siku saba na kuwahudumia zaidi ya wananchi 3,000. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Polisi yatoa elimu ya utapeli 'tuma kwa namba hii'

**Na Halfani Chusi**

JESHI la Polisi limeingia mtaani kutoa elimu kwa umma ili kukomesha vitendo vinavyofanywa na matapeli wanaotuma ujumbe mfupi usemao 'tuma kwa namba hii'.

Matukio ya utapeli wa namna hiyo yamekuwa yakiwasababishia wananchi hasara kutokana na kujikuta wakituma fedha kwa matapeli bila kujua kutokana na baadhi yao hujitambulisha wanatoka katika mitandao ya simu.

Kutokana hali hiyo, mara kadhaa Jeshi la Polisi limekuwa likiwakamata wanaodaiwa kujihusisha na utapeli huo na hata wengine kufikishwa mahakamani.

Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Polisi, Beatrice Charles, akitoa elimu hiyo juzi kwa wananchi maeneo ya Mikocheni mkoani Dar es Salaam, aliwataka wananchi kutoa taarifa kwa polisi pale unapotokea uhalifu ili kufahamu namna ya kuwapata wanaojihusisha na utapeli mtandaoni.

Aliwataka wenye taasisi, kampuni kutunza vizuri taarifa za wafanyakazi wao, kwani wasipofanya hivyo kutoa mwanya kwa matapeli kuhakiki taarifa zao na kuwatapeli.

"Pia watumiaji wa simu wanapaswa kuhakiki taarifa za watu wanaowapigia simu na kusema 'tuma pesa kwa namba hii' au 'nimetuma pesa kimakosa'" alisema Beatrice.

Alionya kitendo cha wananchi kushiriki katika masuala ya kihalifu akisisitiza kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Inspekta Msaidizi wa Jeshi la Polisi Waziri Makang'ila, alisema kosa la utapeli huingia kwenye jinai kwa kuwa linakiuka sheria za nchi, huku akisisitiza mtu akifanya kosa hilo lazima atakamatwa.

"Tunasema hivi, jambo lolote mhalifu anapolifanya lazima aache kitu cha kumtambulisha, kama kapita mlangoni lazima kuna kitu atakuwa kashika.

# Serikali yasisitiza fedha za umeme kufikisha huduma kwa wananchi

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Waziri wa Nishati, Judith Kapinga, amesema suala la umeme ni ajenda ya kimkakati ya serikali, hivyo watahakikisha wanasimamia rasilimali fedha zinazotolewa ili zitumike kama zilivyokusudiwa kufikisha umeme kwa wananchi.

Amesisitiza kwamba, serikali ipo kazini kuhakikisha ajenda hiyo inatekelezwa kwa ufanisi mkubwa kupitia miradi mbalimbali kwa kufikisha nishati maeneo yote nchini ikiwamo katika vijiji na vitongoji.

Judith aliyaeleza hayo jana alipotembelea Vitongoji vya Migwala na Oloodo Larkaria, Kata ya Sepeko, wilayani Monduli, mkoani Arusha, ambako akiwatoa hofu wananchi ambao huduma hiyo haijafika katika maeneo yao, kwamba watahakikisha inafika kwa wakati.

"Ili umeme ufike katika vitongoji ni lazima kwanza ufike katika vijiji vyote, na hadi sasa vimepata umeme vijiji visivyozidi 70 nchini.

"Tayari vijiji vyote 368 vilivyoko katika Mkoa wa Arusha vimepata umeme na vitongoji 981 kati ya 1,656 vimefikiwa na huduma hiyo," alisema Judith.

Alisema hatua za kufikisha huduma hiyo katika maeneo hayo ikiwamo Kitongoji cha Lindikinya na Larkaria, tayari mkandarasi ameshapatikana na yupo katika hatua ya manunuzi, huku akitarajiwa kuanza utekelezaji wa mradi hivi karibuni.

Alisema baada ya miradi ya umeme kukamilika katika eneo hilo, wananchi wataongeza shughuli za uzalishaji pamoja na kuchochea matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Naibu Waziri huyo amehamasisha Watanzania kujiepusha na matumizi ya nishati chafu ya kupikia badala yake watumia umeme na gesi.

Akiwa katika Shule ya Msingi Lukas Muhina, Kijiji cha Losurwa, Kata ya Esilalei, Judith alisema Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati Dk. Doto Biteko, alimwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kutenga Sh. milioni 300.

Alisema fedha hizo ni kwa ajili ya kufikisha umeme shuleni hapo, huku matarajio yakiwa ni kunufaisha shule hiyo pamoja na maeneo jirani.

## HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.



**Mtunzi Adam Fungamwango (0716 350534)**

# Damu ya Mariamu-**42**

Materu alivyotembeza pesa kwa madaktari na polisi pia. Dokta Shija alimtambulisha kwa mdogo wake afande Willy, na wote kwa pamoja watatu ndiyo kwa kiasi kikubwa waliingia kazini kusaka ukweli wote. Na kwa ujuzi wa hali ya juu wakiongozwa na afande Willy, wakifanikiwa kukusanya ushahidi wote na kuuleta mahakamani ukiwa haina shaka yoyote." Jaji alikuwa katika hatua za mwisho.

"Baada ya kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, mahakama kwa kauli moja imeridhika na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, hivyo kuwatia hatiani watuhumiwa wote wanane waliohusika na tukio hilo.

Hukumu ni kama ifuatavyo. Mshtakiwa namba moja, Boniphace Materu, mashtakiwa namba tatu hadi namba nane, wote wanahukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kuhusika, kushiriki, kuratibu na kupanga njama za mauaji ya marehemu Mariamu kwa makusudi kwani. Haki ya rufaa ipo kwa siku zisizozidi 30. Mashtakiwa namba mbili yeye anahukumiwa kunyongwa mpaka kufa kwa kosa la kumuua kwa kumpiga kitu kizito kichogoni. Na yeye na haki ya kukata rufaa kabla ya siku 30 kuanzia sasa." Akamaliza Jaji Mahundi.

Mazingira ya mahakama yalibadilika. Kutoka kuwa kimya kana kwamba watu wako kwenye ibada kulisikika makofi, mayowe, vigelegele na shangwe kutoka kwa umati wa watu uliofurika ndani ya nje ya mahakama. Hata hivyo kulikuwa na kundi dogo lililomezwa na watu wengi waliokuwa wakishangilia. Wao waliangua vilio. Walikuwa ni baadhi ya ndugu wa wahukumiwa hao.

Mahakama ilimaliza kazi yake. Waandishi hasa wapiga picha nao walianza kazi yao ya kushuti na kupiga picha chochote ambacho waliona kinaweza kuvutia watazamaji kwenye televisheni, blogu na magazeti yao.

Kati watu waliopata bahati ya kijipenyeza kwenye madawati yaliyokuwa ndani ya mahakama ni Kamal, mchumba na marehemu Mariamu. Mwingine ni Afande Willy. Kaka yake Dokta Shija naye alikuwepo. Hawakukaa sehemu moja. Kila mmoja walikuwa amekaa sehemu yake kutokana na mazingira yaliyokuwemo ndani ya mahakama. Hukumu ilipotoka walitafutana. Wakakutana. Wakakumbalia.




Waandishi na wapiga picha nao hawakuwa mbali. Waliwapiga picha za video na mnato. Wao walionekana kama mastelingi. Waliombwa na baadhi ya wandishi kwa ajili ya kuulizwa maswali mawili matatu. Walikubali. Walijibu kile ambacho waliona kinafaa kujibiwa na kile ambacho waliona hakifai kwa manufaa ya umma, au kulinda usiri walikwepa.

Baada ya kumaliza walitafutana tena. Wakakutana. Wakakumbatiana tena "Dokta Shija, nashukuru sana kwa kila ulichofanya juu yangu. Wewe ndiye kwa kiasi kikubwa umetufikisha hapa. Tangu siku ile hospitali nilipokutana na wewe na nikafahamu kuwa ulikuwa mmoja wa ulioufanyia uchunguzi mwili wa mpenzi wake nikajitambulisha, hukunitupa, unanionyesha kila aina ya upendo. Uliahidi kunipa msaada. Si wa kunificha tu bali hata kunisaidia ili kuusaka ukweli. Unanikutanisha na mdogo wako afande Willy. Na leo tuko hapa. Sina cha kusema sina cha kukulipa dokta. Atakulipa Mungu mwenyewe. Ila tangu leo mdogo wako si Willy peke yake. Mimi pia nitakuwa mdogo wako." Akasema Kamal huku akikumbatia kwa nguvu Dokta Shija.

"Usijali Kamal. Wewe ni kijana wa pekee. Kijana jasiri. Usiye wa woga, mwenye tabia ya kipolisi. Tabia ya kipelelezi. Mimi niliiona nia yako ya dhati ya kusaka wauaji. Na kwa jinsi ulivyokuja hospitalini kwangu kwa hila kama askari mpelelezi hadi ulipojitambulisha mwenyewe. Na kwa vile tayari mkasa huu nilikuwa nimeshaanza kuufahamu kuwa umezungukwa na hila. Niliamua kukusaidia na wewe nikajua utajisaidia pia. Ndiyo maana nikakutanisha na mdogo wangu Willy. Kusema kweli mmefanya jambo la kishujaa. Mmefanya kazi ambayo ilitakiwa kufanywa na watu wengine, lakini kwa makusudi na rushwa hawakufanya. Leo mmeliheshimisha Jeshi la Polisi. Pongezi hizi si za kwangu tu. Ni zetu sote." Dokta Shija alijibu pongezi za Kamala. Akamgeukia afande Willy. "Yamekwisha kamanda. Kazi tuliyoifanya tumeimaliza. Nashukuru sana kwa plani, mipango, na kuongoza operesheni yote ya kusaka vielelezo na vitu ambavyo vimetuwezesha kwanza kuwapata wahusika, lakini pamoja na ushahidi uliowatia hatiani. Vinginevyo tunepata tabu sana."

"Kamal, hii ni kazi yangu, na niliifanya baada ya kuhadithiwa na kaka yangu juu ya mpango huu usio wa kiutu wala kibinadamu. La pili nilipokutana na wewe, tabia ya vitendo vyako vilionyesha kuwa naweza kufanya kazi kwa kukushirikisha wewe pia na siyo mimi peke yangu. Umeifanya kazi hii kiueledi kana kwamba nilikuwa nafanya kazi ya askari polisi si mpelelezi tu, ila ni komandoo pia." Alisema na kusababisha vicheko kwao wawili.

**Mahakama ilimaliza kazi yake. Waandishi hasa wapiga picha nao walianza kazi yao ya kushuti na kupiga picha chochote ambacho waliona kinaweza kuvutia watazamaji kwenye televisheni, blogu na magazeti yao.**

"Kamal, sitojali kama nitafukuzwa kazi, kwani nimeifanya kazi hii bila ruhusa yao. Pamoja na kwamba wameonekana kuniunga mkono na kupeleka ushahidi mahakamani, lakini kisheria ni kwamba niliifanya bila kibali, sijajua wataamua nini, lakini hapa nilipo moyo wangu ni mweupe, dunia nzima imenifahamu na imejua nimefanya hivi na manufaa ya nchi. Wewe ni rafiki yangu mwema, utaendelea kuwa rafiki yangu daima." Kamal na Willy walikumbatiana. Wote watatu sasa wakawa wanaelekea kwenye gari na Dokta Shija.

Ghafla Kamal akajikuta amekumbatiwa kwa nguvu na mtu ambaye hamfahamu. Hata hivyo mtu aliyemkubatia alionekana kuwa na mwili laini uliomfariji kwa kiasi fulani.

"Shemeji Kamal." Ilisikika sauti ambayo iliita jina lake na kulia. Mtu aliyemkubatia na kuanza kuangua kilio ni Teddy. Huyu ni ndogo wa marehemu Mariamu. Kumbe naye alikuwa mahakamani. "Teddy!" Akaita Kamal.

"Nilijua na wewe umekufa shemeji yangu!" Aliendelea kulia.

""Nyamaza Teddy, isingewezekana kufa kabla sijatimiza ahadi yangu niliyoiweka. Nilikwambia siku ile wakati nakuaga kuwa ni lazima nimpate muuaji wa dada yako Mariamu. Na nyingine unaijua mwenyewe." Maneno hayo yalimfanya Teddy kwanza ananyue kichwa na kumtazama Kamal, lakini kwa aibu kwani macho yake yalishindwa kuendelea kutazama zaidi.

"Umekuja na nani?" "Nimekuja na ndugu zangu wote." "Mbona hawakuja kuniona." "Shemeji wewe mwenyewe unajua kilichotokea nyuma. Wale wote walikuwa wanakushutumu na kukuhisi kuwa wewe ni kweli umemuua dada kama ambavyo askari walivyobainisha. Unajua ni mimi peke yangu nilikuwa siamini na nisingemini kamwe. Na nilipata lawama na kutoaminiwa na ndugu zangu kwa sababu hii ya kukutetea, leo ukweli umedhihirisha Tena ni wewe mwenyewe ndiye uliyekuwa ukisaka ukweli. Haiwezekani kirahisi zaidi waje hapa. Bado wana aibu. Itachukua muda kidogo.

"Basi mama, ngoja niondoke na hawa jamaa zangu. Baada ya siku mbili nitakutafuta nina kesi na wewe ujue."

Teddy akatabasamu. Akamuacha Kamal aliyekuwa amemkumbatia. Akaachia tabasamu zito wakati bado machozi yalikuwa hayajakauka mashavuni.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# NAMUNGO YAMGEUKIA AMOAH

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kutofanya vyema katika mechi nyingi za mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, klabu ya Namungo imeanza kukiongezea nguvu kikosi chake baada ya kufanya mazungumzo ya kumsajili kiungo wa zamani wa Azam FC, Daniel Amoah.

Habari kutoka ndani ya klabu hiyo inasema tayari mazungumzo na kiungo huyo mkabaji anayeweza pia kucheza kama beki wa kati yamekamilika kwa asilimia 90, hivyo kuna uwezekano mkubwa raia huyo wa Ghana kuichezea Namungo kuanzia mzunguko wa pili.

"Kama unavyoona hatujafanya vyema sana karibu mzunguko wote huu wa kwanza, kwa maana hiyo ni lazima tuongeze watu, Namungo hii siyo ile ambayo watu wanaijua, tunataka mzunguko wa pili tufanye marekebisho kadhaa, kwa kuanzia tunaanza upande wa ulinzi, tumezungumza na Amoah, yule ambaye alikuwa akiichezea Azam. Anacheza nafasi ya kiungo mkabaji, hata beki wa kati, nadhani atatusaidia, huku tukiwa tunaangalia maeneo mengine. Tukishakamilisha kila kitu sasa ndiyo tutatoa taarifa rasmi kwa waandishi wa habari," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo.

**Kiungo huyo aliingia nchini mwaka 2016 akisajiliwa na Azam, kutokea klabu ya Medeama ya Ghana baada ya kuonekana kwenye mechi mbili za Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi dhidi ya Yanga.**

Mechi ya kwanza iliyochezwa, Julai 16, 2016 nchini, Medeama na Yanga zilitoka sare ya bao 1-1, kabla ya Julai 26, mwaka huo, timu hiyo ya Ghana kushinda mabao 3-1, akionyesha uwezo mkubwa kwenye mechi hizo, na kupelekea mabosi wa Azam kuvutiwa na kiwango chake.

Aliitumikia Azam kwa miaka minane kabla ya kuachwa mwishoni mwa msimu uliopita.

Namungo inashika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, ikiwa na pointi tisa baada ya kucheza michezo 12.

## *Magari kushindaniwa 'magifti ya kujifti'*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Yas jana imezindua awamu ya pili ya kampeni ya magifti ya kujifti ambapo imetoa magari mapya mawili kwa ajili yakushindaniwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo wa pili jijini Dar es salaam, Ofisa Mkuu wa Mixx by Yas, Angelica Pesha, alisema awamu hiyo inatoa fursa kwa wananchi kujaribu bahati yao ambapo mbali na magari hayo pia zawadi mbalimbali ikiwemo fedha zitatolewa wakati wa kampeni hiyo.

"Magift ya Kugift ni ishara yetu ya shukrani kwa wateja na washirika wetu na wananchi kwa ujumla wanaofanya Mixx by Yas kuwa ya kipekee. Tunapoingia Awamu ya Pili, tunafurahia kuleta fursa zaidi zinazobadilisha maisha kwa jamii yetu. Hii si kampeni tu, bali ni sherehe ya mshikamano na furaha ya pamoja, tunapofunga mwaka kwa kutoa shukrani kwa dhati." alisema Angelica.

Kwa upande wake, Afisa Mkuu wa Biashara wa kampuni hiyo, Isaack Nchunda, alisema kampeni hiyo inaonyesha dhamira yao yakurudisha kwa jamii kile wanachokipata.

"Kampeni hii inaonyesha dhamira yetu ya dhati ya kunda uzoefu wenye maana kwa watu wetu. kazi ipo kwao kushiriki kuweze kushinda," alisema.

Aidha, Msemaji wa kampeni hiyo ambaye ni msemaji wa zamani wa klabu ya Yanga, Haji Manara, amewataka wananchi kushiriki kuweza kushinda zawadi mbalimbali.

"Ukitoa magari, kuna zawadi ya fedha mpaka shilingi milioni 50, watuwanaweza wakafunga mwaka kwa tabasamu kubwa kutoka Yas," alisema Manara.



Msemaji wa zamani wa klabu ya Yanga, Haji Manara ambaye kwa sasa ni msemaji wa kampeni ya Magifti ya kujifti akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo. **PICHA: FAUSTINE FELICIANE**

## Ndafu Festival kunogesha Rombo Marathon 2024

**Na Romana Mallya**

MBUNGE wa Rombo na Mwenyekiti wa Rombo Marathon, Adolf Mkenda, amewataka wadau na wanariadha mbalimbali kujitokeza kwa wingi kushiriki mbio hizo zitakazopambwa na 'Ndafu Festival'.

Akizungumzia mbio hizo jana, Mkenda alisema linatarajia kwenda sambamba na bonanza la kuchoma nyama na litafanyika kwa siku tatu mfululizo kuanzia Desemba 23 wilayani Rombo, mkoani Kilimanjaro.

"Mwaka huu, kama kawaida tutakuwa na duru ya tatu ya bonanza la michezo na tamasha la nyama choma, vyakula vya asili kama ng'ande, ngararimo, mbege nzuri na vinywaji vingi vitakuwepo, Rombo Marathon na Ndafu Festival itafanyika Desemba 23, mwaka huu, kuanzia viwanja vya Kirombero Rongai ambapo kutafanyika marathon, watu watakimbia kuanzia kilometa tano, kilometa 10 na kutembea msituni kwenye kiza kinene na mandhari za kuvutia, alisema Mkenda.

Aidha, alisema wanawakaribisha watu wote kushiriki ili kujenga afya zao.

Mkenda alisema mbio hizo hutumika kufadhili shughuli mbalimbali, ambapo kwa mwaka jana, fedha zilitumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya elimu na afya katika hospitali ya Huruma pamoja na shule za serikali.

"Tutaendelea kukamilisha ujenzi wa vyoo vya shule za serikali katika Wilaya ya Rombo. Ninakaribisha Watanzania wote, nimepata taarifa kuna wenzetu kutoka Botswana wanataka kuja kukimbia. Wakenya wanakuja kwa wingi kushiriki marathon na kujifua na kujichana," alisema.

**Tutaendelea kukamilisha ujenzi wa vyoo vya shule za serikali katika Wilaya ya Rombo. Ninakaribisha Watanzania wote, nimepata taarifa kuna wenzetu kutoka Botswana wanataka kuja kukimbia.**

## ZISIKUPITE

### AZIVUTIA ARSENAL, N'CASTLE

ARSENAL na Chelsea zinamtafuta mshambuliaji na klabu hizo mbili za London zina orodha sawa ya wachezaji wanaowataka, ambayo ni pamoja na mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak, 25. ***(Caught Offside)***

### FOWADI KIPAUMBELE MAN

KLABU ya Manchester United imefanya usajili wa mshambuliaji kuwa kipaumbele chake katika dirisha la usajili la Januari. ***(Mirror)***

### DAVIES KUSAINI BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inajiandaa kumuongeza mkataba mchezaji wao wa kimataifa wa Canada, Alphonso Davies, 24, huku Manchester United wakionesha nia ya kumtaka beki huyo. ***(Floran Plettenberg, Sky Germany)***

### UNITED YAMTAKA DORGU

KLABU ya Manchester United ipo kwenye mbio moja na Chelsea katika kuwania kumsajili beki wa Lecce raia wa Denmark, Patrick Dorgu. ***(Team Talk)***

### POTTER KUDAKA KAZI MPYA

KOCHA wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter ameuliziwa na klabu za Wolves na West Ham. ***(Sportsport)***

### DAVID MOYES AITAKA WOLVES

KOCHA wa zamani wa West Ham, David Moyes ni miongoni mwa wanaowania nafasi ya kazi katika klabu ya Wolves iwapo Gary O'Neil atafukuzwa ***(Telegraph)***

### FRIMPONG ATAKIWA L'POOL

LIVERPOOL inawasiliana na Bayer Leverkusen kuhusu uhamisho wa beki wa Uholanzi, Jeremie Frimpong, 23. ***(Caught Offside)***

### KURUHUSIWA KUONDOKA

KLABU ya Manchester City itamruhusu kiungo wa Ubelgiji, Kevin De Bruyne, 33, kujiunga na moja ya klabu dada za Man City Football Group atakapoondoka kwenye kikosi hicho. ***(Telegraph)***

### BETO, DOUCOURE WASAKWA

MSHAMBULIAJI wa Everton na Guinea-Bissau, Beto, 26, na kiungo wa Mali, Abdoulaye Doucoure mwenye miaka 31, wanasakwa na klabu ya AS Roma. ***(Gazzetta dello Sport)***

### KUSAINI MKATABA MPYA

LIVERPOOL ina uhakika mlinzi wa Ufaransa, Ibrahima Konate, 25, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo huku mazungumzo yakiendelea kuhusu mkataba mpya. ***(Fabrizio Romano)***

### BADIASHILE AWANIWA ITALIA

JUVENTUS na Marseille zinawania kumsajili beki wa Chelsea, Benoit Badiashile, 23. ***(Caught Offside)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MUSIALA KUSAINI MKATABA MPYA BAYERN MUNICH

**MUNICH,** Ujerumani

JAMAL Musiala anatazamiwa kusaini mkataba mpya na Bayern Munich ili kumaliza hali ya sintofahamu kuhusu mustakabali wake, ripoti imefichua.

**Musiala ni mmoja wa wachezaji chipukizi bora katika soka la dunia na hali ya mkataba wake wa sasa umebakiza miezi 18 tu kukamilika na klabu kadhaa za Ulaya zinawania saini yake.**

●●● Hatua hiyo itamaliza sintofahamu kuhusu mustakabali wake ndani ya.....

Real Madrid na Manchester City wametawala vichwa vya habari kuhusiana na uwezekano wa kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, lakini pande zote mbili zinatazamiwa kukatishwa tamaa kwa kuwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani sasa anatarajiwa kusaini mkataba mpya na Munich.

Sky Sport Ujerumani inaeleza makubaliano ya jumla yamefikiwa kati ya Bayern na Musiala na kilichobaki ni kuamua urefu wa mkataba huo mpya.

Musiala atatia wino mkataba wa miaka minne wenye thamani ya euro milioni 100 au mkataba wa miaka mitano wenye thamani ya euro milioni 125.

Pia kunatarajiwa kuwa na bonasi kubwa ya kusaini na ada ya wakala ambayo inaweza kuongeza euro milioni 20 nyingine.

HABARI MICHEZO

# POSTECOGLOU AWATULIZA MASHABIKI SPURS



**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou amewatuliza mashabiki baada ya timu yake kufungwa bao 1-0 na Bournemouth juzi kwenye Ligi Kuu ya England jambo ambalo liliongeza shinikizo kwa raia huyo wa Australia.

Kikosi cha Postecoglou hakikuweza kutambulika kutoka kile ambacho kiliilaza Manchester City mabao 4-0 katika mchezo wao wa mwisho wa ugenini, na hivyo kusababisha matokeo duni.

Sasa wamepoteza mechi sita kati ya 14 za ligi msimu huu na wako katika nafasi ya 10, chini ya Bournemouth.

Mashabiki walimzomea kocha baada ya filimbi ya mwisho na Postecoglou ilishirikisha wachache kwenye mazungumzo.

"Wamekata tamaa, ni sawa. Walinipa maoni ya moja kwa moja ambayo nadhani yanachukuliwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

Alipoulizwa ni nini kilizungumzwa, aliongeza: "Labda sio kwa hapa. Sina shida nayo. Sikupenda kilichosemwa kwa sababu mimi ni binadamu.

"Nimekuwepo kwa muda wa kutosha kujua kwamba ikiwa mambo hayaendi vizuri, lazima uelewe kuchanganyikiwa."

Postecoglou anakabiliwa na wiki chache muhimu wakati kikosi chake kinawakaribisha Chelsea kesho Jumapili na kusafiri hadi Rangers kwa mechi muhimu ya Ligi ya Europa wiki ijayo.

Baada ya safari ya kuelekea kucheza dhidi ya Southampton na baadae dhidi ya Manchester United katika robo fainali ya Kombe la Ligi na kuwakaribisha vinala wa Ligi, Liverpool siku chake kabla ya Krismasi.

## Roque: Nilifikiria kukataa kwenda Real Betis

**BARCELONA,** Hispania

VITOR Roque amefichua kwamba alifikiria kujitoa na kurejea katika shamba lake dogo nchini Brazil wakati wa kipindi kigumu akiwa Barcelona.

Fowadi huyo wa Brazil alikiri kwamba alipoteza imani yake na Barca, ambayo alijiunga nayo Januari kutoka Athletico-PR kwa mkataba wa awali wa euro milioni 35.

Sasa akiwa anacheza kwa mkopo wa muda mrefu katika klabu ya Real Betis, Roque aliiambia ESPN, "Wakati mgumu zaidi ni ule niliopitia pale Barcelona. Lakini namshukuru Mungu, nilikuwa na familia yangu kando yangu. Ikiwa huna furaha na kama huna kujiamini, mambo hayaendi sawa.

"Wakati fulani nilizungumza na mama yangu na kumwambia 'sihitaji chochote kati ya hayo, nahitaji kuwa na furaha, ambalo ndilo jambo muhimu zaidi.' Lakini wakati mwingine unapaswa kupitia mambo kama haya ili kujifunza, kushinda."

Alipoulizwa ikiwa alifikiria kukata tamaa, alisema: "Ndiyo. Nilifikiri ninataka kwenda shambani Brazil na kuwa mtulivu, bila mtu yeyote kunitia wasiwasi, kwa sababu wakati mwingine ni vigumu shiniki linakuwa kubwa.

"Lakini ni kuhusu kusonga mbele tu, kuwa na nguvu za kiakili, kuendelea kufanya kazi kwa unyenyekevu mkubwa na mambo yanakuwa mazuri kidogo kidogo, ninapata furaha yangu kamili na kujiamini pia," alisema.

Barca iliweka kipengele cha kutolewa cha euro milioni 500 katika mkataba wa Roque, huku matarajio yakiwa makubwa kwa mchezaji huyo ambaye alikuwa na kiwango cha kuvutia akiwa Athletico-PR na timu za vijana za Brazil.

# Makundi klabu bingwa Dunia yawekwa hadharani

**MIAMI,** Marekani

DROO ya Klabu bingwa ya Dunia ya FIFA imepangwa juzi na mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City wamepangwa na Juventus, Wydad Casablanca na Al Ain kwenye Kundi G michuano itakayofanyika mwakani nchini Marekani.

Lionel Messi na timu yake ya MLS Inter Miami wako katika Kundi A na watamenyana na Al Ahly katika mechi ya ufunguzi wa michuano hiyo iliyopanuliwa hadi timu 32 kabla ya mechi dhidi ya Porto na Palmeiras.

Mashindano hayo, yanayoshirikisha klabu bora kutoka mabara yote, yatafanyika katika viwanja 12 nchini Marekani kuanzia Juni 15 hadi Julai 13 na kutumika kama mandazlizi ya Kombe la Dunia la 2026 linaloandaliwa na nchi tatu, Marekani, Mexico na Canada.

Miongoni mwa klabu kubwa duniani ni Real Madrid, Bayern Munich, Paris Saint-Germain, Chelsea, Borussia Dortmund na Inter Milan. Pia kuna timu nne kutoka Amerika Kusini ambazo ni Flamengo, Palmeiras, River Plate na Fluminense.

Timu ya Messi, kama mwakilishi wa taifa mwenyeji, inapata sifa ya kucheza mechi ya kwanza ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Hard Rock huko Miami Gardens, Florida.

"Inahusu ushirikishwaji, ni kuleta klabu kutoka duniani kote, klabu 32 bora na wachezaji bora kutoka kote ulimwenguni," alisema Rais wa FIFA, Gianni Infantino.

Mechi zingine za ufunguzi ni pamoja na PSG dhidi ya Atlético Madrid na Monterrey dhidi ya Inter Milan katika Kundi E na Real Madrid wakikabiliana na klabu ya Saudi Arabia Al-Hilal katika Kundi H pambano la nyota bora, Kylian Mbappé wa Real Madrid na uwezekano wa kukutana na Neymar wa Al-Hilal.

Manchester City ilishinda Klabu bingwa ua Dunia mwaka 2023 chini ya muundo wa zamani na wako nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu England.

Timu kutoka Brazil Botafogo ilifanikiwa kutinga fainali wiki iliyopita kwa kushinda taji lao la kwanza la Copa Libertadores (Ligi ya mabingwa Amerika Kusini)_.

Chelsea wataanza mechi ya Kundi D dhidi ya Leon kabla ya kumenyana na Flamengo na Esperance, huku Kundi F likiundwa na timu za Fluminense, Borussia Dortmund, Ulsan HD na Mamelodi Sundowns.

Mashindano ya klabu yanatumia muundo wa jadi wa timu 32 uliotumiwa na Kombe la Dunia kutoka mwaka 1998 hadi 2022.

Makundi nane ya timu nne nne kila moja yalipangwa na timu mbili za juu kutoka kila kundi zikisonga mbele hadi hatua ya mtoano ya 16 bora.

Ulaya imetoa timu 12 na Amerika Kusini sita, wakati Afrika, Asia na Amerika Kaskazini zote zimetoa timu nne na Inter Miami kimsingi ikiwa ya tano kutoka Amerika Kaskazini kwani ina hadhi ya mwenyeji na bara la Oceania ilipata nafasi moja.

Droo hiyo iliyofanywa na mshindi wa Kombe la Dunia la Italia na nguli wa zamani wa Juventus, Alessandro Del Piero, ilijumuisha ujumbe uliorekodiwa kutoka kwa Rais mteule wa Marekani, Donald Trump.

"Tukio hilo litakuwa la kushangaza. Nitajaribu kuwa hapo. Nikiweza, tutaona kitakachotokea," alisema Trump.

**Droo kamili ya Klabu bingwa ya Dunia:**

**Kundi A:** Palmeiras, Porto, Al Ahly, Inter Miami.

**Kundi B:** Paris Saint-Germain, Atletico Madrid, Botafogo, Seattle.

**Kundi C:** Bayern Munich, Auckland City, Boca Juniors, Benfica.

**Kundi D:** Flamengo, ES Tunis, Chelsea, Leon.

**Kundi E:** River Plate, Urawa, Monterrey, Inter Milan.

**Kundi F:** Fluminense, Borussia Dortmund, Ulsan, Mamelodi Sundowns.

**Kundi G:** Manchester City, Wydad, Al Ain, Juventus.

**Kundi H:** Real Madrid, Al-Hilal, Pachuca, Salzburg.

HABARI MICHEZO

## Yanga: Tutabeba pointi 3 muhimu

INATOKA UKURASA 24

kwa nidhamu wakati wote watakapokuwa na mpira.

"Hatutarajii mchezo mwepesi, lakini tumejipanga kukabiliana nao lengo letu la kwanza likiwa ni ushindi ili kupata pointi tatu, tutapambana muda wote wa mchezo," alisema mchezaji huyo.

Kennedy Musonda, mshambuliaji wa kimataifa wa timu hiyo kutoka Zambia alisema anaamini wana uwezo wa kuifunga MC Alger licha ya kucheza ugenini.

Musonda alisema kila mchezaji yuko tayari kuipambania timu hiyo na anaamini watawapa furaha wanachama na mashabiki wao.

"Tunaamini tunaweza kuwafunga MC Alger wakiwa kwao, hakuna kinachoshindikana, tutapambana na tunaweza kupata ushindi, tunahitaji sana pointi tatu ili kuendelea kuweka hai malengo yetu ya kucheza hatua ya robo fainali," alisema Musonda.

Baada ya mchezo huo Yanga itasafiri kuifuata kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), kuifuata TP Mazembe ili kukamilisha mzunguko wa kwanza wa kundi lao.

Al Hilal yenye pointi tatu ndio vinara wa kundi hilo wakifuatiwa na MC Alger, TP Mazembe zenye pointi moja kila mmoja huku Yanga ikiburuza mkia.

## Simba yawapania

INATOKA UKURASA 24

Constantine, mwalimu ameshatupa mbinu ambazo zitatusaidia katika mchezo husika, hali ya hewa siyo rafiki sana, ni baridi lakini haitusumbui sana kwa sababu si mara ya kwanza Simba kuja hapa (Algeria), haitakuwa mechi ya kwanza kucheza katika hali kama hii, kwa ujumla maandalizi ni mazuri ya kwa asilimia kubwa yamekamilika.

Nakumbuka mara ya mwisho tulipokuja hapa hatukupata matokeo mazuri ilikuwa ni dhidi ya JS Saoura, lakini ule ulikuwa ni mwaka mwingine na huu ni mwingine pia, na benchi la ufundi sasa ni jipya kabisa, naamini matokeo yetu safari hii yatakuwa mazuri," alisisitiza nyota huyo.

Simba ilicheza dhidi ya JS Saoura Machi 9 mwaka, 2019 kwenye Uwanja wa Agosti 20, mjini Bechar na Wekundu wa Msimbazi walichapwa mabao 3-0.

Katika mchezo wa kesho, mechi ya Simba iliyoko Kundi A itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui ulioko katika Mji wa Constantine.

Timu zote mbili zilishinda katika michezo yao ya kwanza, Simba ikipata ushindi wa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Bravo do Maquis kutoka Angola huku CS Constantine ikivuna pointi tatu ugenini dhidi yaCS Sfaxien ya Tunisia.

# SINGIDA, AZAM DIMBANI MICHUANO KOMBE LA FA

**Na Adam Fungamwango**

RAUNDI ya tatu ya mashindano ya Kombe la FA inatarajiwa kufanyika leo kwenye viwanja mbalimbali nchini kwa ajili ya kusaka bingwa atakayeiwakilisha Tanzania Bara katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

**Jumla ya mechi 14 zinatarajiwa kupigwa leo kwa ajili ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayochezwa kwa mfumo wa mtoano.**

Kwenye Uwanja wa Liti Singida, Singida Black Stars itakuwa mwenyeji dhidi ya timu inayoshiriki First League (zamani Ligi Daraja la Pili), Magnet FC.

Ofisa Habari wa Singida Black Stars, Hussein Massanza, amesema itakuwa ni fursa nzuri kwa mashabiki wa timu hiyo kuwaona wachezaji wao baada ya kuwakosa kwa muda mrefu.

"Mara ya mwisho kucheza kwenye uwanja wetu, ilikuwa Oktoba 25, mwaka huu tulipocheza dhidi ya Fountain Gate na tuliondoka na ushindi wa mabao 2-0, tunarudi tena kuwapa furaha mashabiki wetu ambao wameimisi kwa muda mrefu, tunawakaribisha sana kuiona tena timu yao kwenye Uwanja wa Liti, Singida. Tutakutana na Magnet," alisema Massanza.

Kwenye Uwanja wa Ilulu, Iringa, wenyeji Bigman FC watawakaribisha Soccer City huku Trancsit Camp itakuwa kwenye Uwanja wa Mabatini, mkoani Pwani kupepetana na Gunners FC wakati Biashara United itakuwa kwao, Musoma kwenye Uwanja wa Karume kuvaana na TRA FC.

Michezo mingine itapigwa, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro, Mtibwa Sugar itacheza dhidi ya Greenland, Songea United itakuwa kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea kuikabili Kidudi FC huku Mashujaa FC itawaalika Tukuyu Stars kwenye dimba la Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

KMC ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam itakipiga dhidi ya Black Six wakati Pamba Jiji itashuka kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza kuvaana na Moro Kids na Fountain Gate utacheza dhidi ya Mweta Sports kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa ulioko Babati mkoani, Manyara.

Azam FC itakuwa mwenyeji wa Iringa Sports kwenye Uwanja wa Azam Complex, Coastal Union itavaana na Stand United jijini Arusha huku Kagera Sugar na Rhino Rangers wakichuana kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba na Dodoma Jiji itacheza dhidi ya Leo Tena.



Magolikipa wa Azam FC (waliopiga magoti), wakiwa na makocha wao baada ya kumaliza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya raundi ya tatu ya mashindano ya Kombe la FA dhidi ya Iringa Sports itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## *Serengeti Boys kamili CECAFA*

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), kimetamba kinakwenda kuteteta ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17), yanayotarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 14 hadi 28, mwaka huu jijini Kampala, Uganda.

Akizungumza kabla ya kuanza safari hiyo jana, Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Boniface Pawasa, alisema kikosi chake kiko tayari kwa ajili ya mashindano hayo ambayo wamejipanga kukutana na ushindani.

Pawasa alisema wamepata maandalizi mazuri na wamecheza mechi mbalimbali za kirafiki ili kuwaimarisha nyota wake na sasa ana imani wanakwenda Uganda kupambana.

"Sisi ndio mabingwa watetezi, tunakwenda kupambana kuhakikisha tunafanya vizuri, kwetu kila mechi ni sawa na fainali, hakuna mechi rahisi na wachezaji wanafahamu hilo.

Jana (juzi), tumemalizia maandalizi yetu kwa kucheza mechi ya kirafiki na timu ya vijana ya Coastal Union (u-20), hii ni kwa ajili ya kukamilisha programu yetu, tumefahamu kila kitu kiufundi na nafasi yetu kabla ya kuanza kwa mashindano," alisema Pawasa.

Aliongeza wanakwenda kupambana kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki Fainali za vijana za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), ambazo zimepangwa kufanyika Machi, mwakani huko Morocco.

Michezo
Jumamosi Desemba 7, 2024
Nipashe



Postecoglou awatuliza mashabiki UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga wakifanya mazoezi ili kujiimarisha kabla ya kusafiri kuifuata MC Alger katika mechi ya Kundi A ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo jijini Algers, nchini Algeria. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga: Tutabeba pointi 3 muhimu

**Na Faustine Feliciane**

## Ramovic atamba kazi imebaki kwa wachezaji wake huku Musonda...

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Yanga wanatarajia kutupa karata ya pili kusaka ushindi kwenye mchezo wa hatua ya makundi dhidi ya wenyeji MC Alger utakaochezwa leo kuanzia saa 4:00 usiku kwa saa za hapa nchini.

**Yanga itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kupoteza mchezo wa kwanza wa hatua hiyo wakiwa nyumbani dhidi ya Al Hilal kutoka Sudan.**

Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, ameweka wazi licha ya kucheza ugenini, kikosi chake kitashuka dimbani kikiwa na mpango mmoja wa kusaka matokeo ya ushindi tu.

Ramovic alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea katika mchezo huo na wachezaji wote wanafahamu umuhimu wa kusaka ushindi katika mchezo huo.

"Tumefanya kila kitu kwenye uwanja wa mazoezi, wachezaji wapo katika hali nzuri na wanafahamu nini nimewaelekeza wafanye, kikubwa tunahitaji ushindi, tunafahamu wenzetu nao wamejipanga kupata ushindi, lakini lazima tupambane kwa sababu tumepoteza mchezo wetu wa kwanza, haitapendeza na huu tuupoteze," alisema Ramovic.

Kocha huyo alisema wataingia uwanjani kwa tahadhari lakini hawatacheza mchezo wa kujilinda muda wote.

"Matokeo ya mchezo uliopita yametupa fundisho na hamasa ya kusaka ushindi mchezo huu, nafahamu mashabiki wengi walimia na matokeo yale, sasa ni nafasi ya kurejesha furaha kwa mashabiki," Ramovic alisema.

Naye nahodha msaidizi wa Yanga, Dickson Job, alisema mchezo huo hautakuwa mwepesi kutokana na aina ya wapinzani wanaokutana nao.

Job alisema licha ya kukutana na timu ambayo pia inahitaji kujiimarisha katika msimamo wa Kundi A, wamejiandaa kucheza

ENDELEA UKURASA 23

# Simba yawapania Waarabu

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Simba, Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr', amesema wachezaji wote wa timu hiyo waliopo Algeria 'wameipania' mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya CS Constantine itakayochezwa kesho nchini humo.

Nyota hao wa Wekundu wa Msimbazi kila mmoja anataka apangwe katika kikosi cha kwanza kwa lengo la kuonyesha ubora wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zimbwe Jr, alisema wachezaji wote wako tayari na hawana hofu hata kidogo kuelekea mchezo huo na kila mmoja amejiandaa vyema kupeperusha bendera ya timu yao.

Beki huyo alisema wachezaji wamedhamiria kufanya vizuri katika mashindano hayo msimu huu ili kuwapa furaha mashabiki wao.

"Hali ni nzuri na kila mchezaji anautamani mchezo, kila mmoja wetu anataka kuwa sehemu ya kikosi cha kwanza ili aoneshe kiwango na uwezo wake, sasa mwalimu Fadlu Davids ndiyo ataamua nani amuweke na nani akae benchi, lakini watakaoanza na watakaoingia kipindi cha pili lengo letu litakuwa moja tu, kupambania nembo ya Simba na Tanzania kwa ujumla," alisema nahodha huyo.

Aliongeza maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yamekamilika kwa zaidi ya asilimia 90, kilichobaki ni vitu vichache ambavyo benchi la ufundi linafanyia kazi.

"Safari ilikuwa ndefu sana, lakini tumefika salama, kikubwa kilichotuleta hapa ni kimoja tu mechi yetu dhidi ya CS

ENDELEA UKURASA 23



Zimbwe Jr akijifua

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002